# *Uponyaji Wa Kiungu*

"...huko ndani. Sina budi kurusha wavu mpaka kila samaki atolewe nje; unajua kila mmoja aliye wako." Alisema...Nilisema, "Nitawatoa, basi wao—wao ni wako basi. Ninawawasilisha kwako." Lakini nikasema, "Hutawatoa hapo isipokuwa uwashike kwa wavu."

2 Na hivyo ndivyo kuhubiri kunavyopaswa kufanya, ni kuwashika kwa wavu. Nasi tunarusha wavu hapa, na labda Bwana aseme, "Naam, tupa wavu wako upande *huu*." Na tungetupa huko, na kuvuta nje. Vema, mle ndani, hatupati, labda, ila samaki mmoja tu, ama wawili, katika wito huo wa madhabahuni. Na labda baadhi yao wanakuja, na kurudi nyuma ulimwenguni, haileti tofauti yoyote kwao. Naam, tulifanya kadiri ya uwezo wetu.

3 Tunaenda kwenye shimo linalofuata, na kutupa wavu wetu ndani na kuvuta kutoka hapo, na kuona tunachoweza kupata katika hilo. Labda tusipate kitu katika hilo. Labda kadhaa wanakuja madhabahuni. Hakuna hata mmoja wao aliyeshikilia; basi hiyo—hiyo ni juu ya Bwana, unaona.

4 Kwa hivyo tunaenda kwenye shimo linalofuata na kutupa ndani, labda tupate kundi zima la samaki kwenye hilo.

5 Tungeona, basi, hata hivyo, unaona, sisi tu—tunaenda tu na kutupa wavu wetu ndani, ni hayo tu. Unaona? Bwana ametuchagua tangu asili kuhubiri Injili, amechagua tangu asili watakaoisikia, kwenye Uzima wa Milele. Sasa hatuna budi kutupa wavu, hiyo ni kweli, unaona, chochote kile—chochote kilicho cha Bwana. Hapa, wote wamelala kuzunguka madhabahu, "Sasa, Bwana, hao hapo. Nimefanya kadiri ya uwezo wangu. Huu hapa wavu wa Injili, umewapata, kila mmoja alinaswa. Unajua samaki ni nini. Na unajua kasa ni nini. Na unajua nyoka ni nini. Na unajua vyura ni nini. Na unajua ni nini, ni nini. Ni Wako, kufanya uchaguzi." Lakini sisi tunatupa tu wavu.

6 Aliiona, lakini hakuikubali. Naam, hiyo ni sawa. Naam, mradi tu wao...unaiwasilisha, sawa.

7 Sasa, inaonekana kana kwamba kila mtu anaimba nyimbo kuhusu Krismasi nyeupe, na kuomba kwa sababu hiyo hiyo. Tunaweza kuwa nayo, inaonekana. Hii inaendelea, tunaweza kuwa na Krismasi nyeupe. Na Krismasi ni wakati wa mwaka...

8 Natamani tu ingekuwa ni Krismasi kila wakati. Kila mtu anaonekana kuwa wa kirafiki sana wakati wa Krismasi, wakitaka kusaidiana, na kila kitu. Kila mtu barabarani, aseme, "Habari yako, kaka?" Nyakati zingine za mwaka, hata

hatazungumza nawe. Kwa hiyo mimi. . .Ingekuwa vyema kama ingesalia Krismasi, (sivyo?) Krismasi tu wakati wote.

9 Na ukweli wa makosa yote na kila kitu kilichoko kuihusu, kuna kitu kuihusu ambacho ulimwengu hujaribu kuifanya X-mas, unajua. Na, lakini Mungu angali ana Krismasi ndani yake, mahali fulani, sivyo? Hakika anayo. Ana jambo fulani juu yake, majina yenyewe tu, na mawazo ya kuzaliwa kwa Bwana Yesu. Loo, ulimwengu umemweka Santa Claus mahali Pake, hakika, lakini si kwa Mkristo. Bado ni Krismasi.

10 Sasa, Krismasi si sherehe ya Kiprotestanti. Ni siku ya Kikatoliki. Tarehe 25 Desemba ilikuwa miezi na miezi kabla ya ninii yetu. . .baada ya. . .au kabla Bwana wetu hajazaliwa. Bwana wetu alizaliwa Aprili. Lakini hakuzaliwa Desemba. Ikiwa umekuwa katika Uyahudi, mnamo Desemba, ni baridi zaidi kuliko hii, kwa hivyo—kwa hivyo unajua Yeye hakuzaliwa Desemba. Na inaandikwa, ni K-r-i-s-m-a-s-i, misa kwa ajili ya Kristo. Ni misa ya Kristo.

11 Tuna sherehe moja tu ya Kiprotestanti Marekani, na Bw. Roosevelt alibadilisha hiyo kwa ajili yetu. Uh-huh. Hiyo ni Shukrani. Zingine zote ni siku za Kikatoliki, kila moja. Unaona? Bw. Roosevelt alitubadilishia hiyo. Kwa hivyo tunayo kila Alhamisi, au wiki fulani, au kitu kama hicho. Haiko kwenye siku iliyowekwa kawaida tena.

12 Kwa hivyo angalia ni kifurushi gani tulichopata! Dunia nzima imekuwa lundo la—la uchafu, na dhambi, na kukata tamaa. Na milele. . .Haina budi kuwa hivyo, kulipuka. Tazama. Jambo hilo lote limetoa vifungo vyote, chuma na kadhalika, kutengeneza meli na madaraja, na kadhalika. Ambacho Mungu alikishikanisha nacho, na kukiunganisha pamoja, na kukiunganisha pamoja hivi; alichukua gesi yote na mafuta na kadhalika, kutoka kwake, namna hiyo, kuchoma, na petroli kwenye magari, na kadhalika. Na kuvuta na kutoa makaa yote, kutengeneza umeme. Unaona? Unaitoa tu, mpaka imekuwa tu ganda, lenye michirizi tu, na kadhalika kutoka kwake namna hiyo. Na ndipo watu wamekuwa tu wenye dhambi sana, mpaka imekuwa tu uchafu mkubwa, mpaka imekuwa tu kama ilivyokuwa mwanzo, "Mungu alihuzunika kwamba alimwumba mwanadamu." Inahitaji tu mtungi mmoja mdogo wa atomiki kuweka kitu kizima katika mpangilio hapo. Yale hasa Yeye alisema angefanya, unaona.

13 Kwa hiyo tunaishi tu katika siku hiyo, na tuna furaha kuwa Mkristo. Loo, jamani! Jamani, ningefanya nini ikiwa mimi. . .Ninaamini ningekuwa wazimu, kama sikuwa Mkristo, nikiangalia jambo hilo. Sioni jinsi watu wanaweza kulistahimili. Sielewi jinsi mwanadamu anavyoweza kutembea duniani, leo, bila kuwa Mkristo. Laiti mtu yeyote angenipa sababu, sababu fulani, kwa nini nisimtumikie Kristo. Mimi—mimi—mimi. . .

Huwezi kutoa sababu ya maana. Unaona? Sisi tu. . .Hii ndiyo siku ambayo sote tunapaswa kuwa na furaha, na tayari, wakati mkuu wa kurudi Nyumbani umekaribia.

14 Na, loo, jamani, kuna tu, "Tene, Tene, Tekel, na Peresi," imeandikwa juu ya kila taifa, kila ukuta, kila mahali. Kila demokrasia, kila ufalme, popote pengine, panaanguka. "Umepimwa katika mizani, ukaonekana umepungukiwa," falme zimepimwa. Wafalme wameanguka. Na madikteta wameanguka. Demokrasia imeanguka. Makanisa yameanguka. Wanadamu wameanguka. Kila kitu kimeanguka.

"Unasema, 'Makanisa'?" Ndiyo, bwana.

15 Moja ya fedheha kubwa kuliko zote duniani ni kanisa. Hiyo ni kweli. Makanisa yameanguka vibaya. Kila kitu kimeanguka. "Lakini tunapokea Ufalme ambao hautaanguka; Yesu Kristo." Hauwezi kuanguka. Nasi tuna furaha sana kwa hilo, kwamba si swala la kanisa. Ni swala la mtu binafsi. Si kama kanisa langu limeokolewa; ni kama nimeokoka. Si kama shemasi wangu ameokoka, ama mchungaji wangu ameokoka, ama mama yangu ameokoka; ni kama nimeokoka, au la. Mimi mwenyewe, lazima niokolewe. Kisha lazima niwaambie. Na halafu, kama wameokolewa, ni ajabu; kama sivyo, ni lazima bado nibaki nimeokolewa. Hiyo ni, lazima nipate wokovu wangu. Loo, siku nzuri jinsi gani!

16 Pia, na—nafikiri, kila siku, karibu sana, kwenye wimbo wa Eddie Perronet, kwamba tumaini langu. . .Hapana, haikuwa Eddie Perronet. Ninasahau ni nani aliyeuandika. "Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu chochote pungufu ya Damu ya Yesu na haki." Huo si ni wimbo mzuri sana? "Yote katika nafsi yangu yanatoweka, na Yeye ndiye tumaini langu na kinga yangu." Unaona? "Juu ya Kristo, Mwamba imara, ninasimama."

17 Wakati maskini Daktari. . .nasahau jina lake, alikuwa. . . alikuwa akihubiri Nguvu za ufufuo wa Kristo, alikuwa katika, unajua, kanisa rasmi mashuhuri katika Jiji la New York, si muda mrefu uliopita. Nilikuwa nayo, kwenye gazeti, ambapo ilikatwa. Na kusanyiko lake lote lilikuwa dhidi yake. Aliamini katika nguvu zisizo za kawaida, ufufuo wa Kristo, Uzima wa Milele, ubatizo wa Roho kumpa mwaminio binafsi Uzima, na ishara na maajabu.

18 Nalo kusanyiko lake lilikuwa likijiandaa kumfukuza. Naye alikuwa na. . .Walikuwa na mapatano ya ukodishaji huko. Alikuwa na chaguo fulani kwamba angeweza kukaa katika kanisa hili kwa muda fulani, na, loo, wananinii tu—wanakaa tu pale na kumkasirisha yule mtu anayehubiri. Lakini alishawishika kuwa alikuwa sahihi. Alikuwa mgonjwa, pia, alikuwa, naye alisema. . .Hapana, hakuwa mtu mgonjwa. Samahani. A—alikufa tu, mimbarani, lakini hakuwa mgonjwa. Hivyo yeye. . .Wao, walimhuzunisha hata kufa. Na kwa hiyo

walimkasirikia tu na hawakutaka kumsikiliza, na kadhalika. Aliendelea tu kuhubiri Kweli. Na wakasema . . .

19 Wao, walikuwa na dini ya kijamii tu, "Loo, tunakuja pamoja. Naye Bibi Jones, hapa, ni wa hapa, kwa hiyo tunakuja pamoja. Tuna karamu zetu ndogo ndogo za chai na kadhalika." Ni mambo ya kijamii tu, lakini aliamini kuwa huo ni upuuzi.

20 "Kwamba, tunapaswa kuja pamoja na kuzaliwa mara ya pili." Nao wakamdhihaki, na kila kitu, kuhusu dini yake, kila kitu.

21 Basi asubuhi moja, nikiwa nimesimama pale, nikilia kwenye mimbara, nikihubiri ya kwamba Yesu Kristo alikuwa halisi, alikuwa na mshtuko wa moyo. Naye a—a—akaanza kuanguka, na akasimama nyuma namna *hiyo*. Na baadhi yao . . . Alikuwa na madaktari kadhaa katika wasikilizaji wake, kwa hiyo wakaja na kumchukua. Waliweka kitu hicho juu ya moyo wake. Wakasema, "Ana mshtuko wa moyo." Wakasema, "Bwana, una—una—unakufa."

Akasema, "Je, ninakufa?"

Kasema, "Naam."

Kasema, "Waombeni mashemasi wangu wawili waaminifu waje hapa."

22 Wakaja karibu na kumwinua. Nao wakasema, "Sasa dini hii mpya, jambo hili unalozungumzia, lina maana gani kwako sasa?"

23 Naye akasema, "Sasa niachilieni." Wakamwachilia. Akainua mikono yake juu. Akasema, "Juu ya Kristo, Mwamba imara, ninasimama! Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao!" Na alipofanya hivyo, alirudi nyuma akiyumbayumba *hivi*. Kulikuwa na msalaba ukining'inia nyuma yake. Alitupa mkono mmoja juu ya msalaba mmoja, na mmoja upande mwingine, namna *hiyo*. Akasema, "Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao! Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao."

24 Akawaza, "Ee Mungu, hiyo ndiyo njia!" Ndivyo hivyo. Ni hayo tu, alikufa msalabani, unaona, kwa . . . Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao. Kristo ndiye tumaini pekee tulilo nalo. Imani yetu haijajengwa juu ya kitu chochote pungufu.

25 Sasa, asubuhi ya leo, nilikuwa naenda kwenye Kitabu cha—cha Waebrania, mlango wa 7. Kwa kuwa nilisikia shuhuda hizi asubuhi ya leo, na haja zetu za maombi, nilifikiri ningeibadilisha tu, kuanzia kufundisha juu ya "Melkizedeki akiwa Kuhani, agizo lililofanywa baada ya kuhani mkuu, adumu Kuhani milele." Na nirudi kule katika Injili, ama Matendo, hasa, na kunena, ama kufundisha, asubuhi ya leo, juu ya *Uponyaji wa Kiungu*, badala yake, kwa sababu ya kuwa na watu wengi sana ambao—ambao ni wagonjwa.

26 Nilisikia tu haja hizo. Nilikuwa nimeketi pale, nikitayarisha, nikisoma, nikichunguza juu ya hii hapa sura ya 6 ya—ya Waebrania, ambapo Melkizedeki Mfalme wa Salemu, Mfalme wa Amani, na kadhalika. Sasa nilianza kusikia yote. . . Nilimsikia, Ndugu Neville, akiuliza kama yeyote. . . Nikaanza kusikia, "Mama yangu; mtoto wangu; *hii* yangu; yangu. . . "

Nikawaza, "Loo!"

27 Kitu fulani kikasema tu, "Rudi kwenye Agano Jipya sasa, kwenye moja ya. . . " Nami nikafungua hapa basi, nikaanza kusoma. Matendo, sura ya 4, ndipo tutakapoanzia asubuhi ya leo, kusoma. Sijui tu ni kwa nini, lakini Roho Mtakatifu akinitaka ni—nibadilishe hili, tena, kufundisha juu ya hili. Bila kujua la kusema, bila shaka, kamwe, bali kujitiisha tu kwa Roho Mtakatifu.

28 Sasa, kila mtu alisikia ambapo mkutano unaofuata utakuwa. Tunaanzia huko—huko Chicago, Kanisa la Filadelfia, na kutoka hapo hadi kwenye jumba fulani la mikutano. Sijui tu ni wapi, bado. Tutaanza tu. Ninaweza kuwa huko kwa siku moja, na ninaweza kuwa huko miezi sita. Unaona? Kuanza tu, na kukaa mpaka Mungu aseme, "Hii imetosha," kisha nahamia mahali pengine. Na tunaanza siku ya 12 ya mwezi ujao, siku ya 12 ya Januari, kwenye Kanisa la Filadelfia huko Chicago. Na ndipo tunatumaini hivi karibuni kuwa Phoenix na huko Magharibi, na pande zote, kama Bwana atakavyotujalia.

29 Nami ninahitaji sana maombi yenu, ninyi watu mniombee. Na mimi. . . si kwa ajili ya afya. Nina shukrani mno na ninashukuru kwa afya yangu njema, Bwana amenipa. Nami nina afya zaidi na bora zaidi, nadhani, kuliko nilivyowahi kuwa na nimekuwa, kwa miaka michache iliyopita. Nami ninamshukuru Mungu Mwenyezi, ambaye Yeye peke yake ndiye aliyenipa, unaona. Maana, kila kitu, mengine yote, yalishindwa tu, na kusema singeweza, nisingeweza hata kufika kwa Mayo. Lakini niko, asubuhi ya leo, kwa neema ya Mungu, nijuavyo mimi, nina afya kamilifu. Kwa hiyo, nina furaha sana kwa hilo. Na kumpa Mungu sifa zote na utukufu wote, maana hakuna kiumbe mwingine, hakuna kitu kingine, kingeweza kufanya hivyo, ila Yeye. Kwa hivyo nina furaha kwa hilo.

30 Lakini, kiroho, na—nahitaji mwongozo wa kiroho. Inaonekana kwangu, wakati wote, kwamba mimi ni mtu aliyeshindwa. Mimi—mimi tu. . . kitu tu kinanisumbua, "Loo, wewe ni usiyefaa." Vema, hiyo, hiyo ni kweli, unaona. Na—najua hilo. Lakini kile kidogo nilicho nacho, nataka kufanya bora niwezavyo kwa kile nilicho nacho. Nami ninatamani mwongozo zaidi wa Roho Mtakatifu, kujua la kufanya, hiyo ni kweli.

31 Maana, baada ya kufikia umri wa miaka arobaini na mitano. . . Bila shaka, ninatambua ninaendelea kusema, "Kuzeeka," lakini huko si kuzeeka. Simaanishi kuwafanya

baadhi yenu ninyi watu, ambao wana umri mkubwa kuliko mimi, kujisikia vibaya. Hiyo ni…Mbona, huyu hapa Ndugu Bosworth katika miaka ya themanini, na mtu bora leo kuliko nilivyo mimi. Lakini ni…Na, tazama, mzee Dk. Ham kule, mwenye umri wa miaka mia moja, naye ni mhubiri mzuri, bado. Kwa hivyo nina njia ndefu, ndefu ya kwenda, kufikia huo. Na nina shaka ikiwa atakubali kuwa yeye ni mzee au la. Kwa hivyo ni ninii tu…

32 Ni, wazo lake ni kwamba, bila shaka, sasa, ningeninii… Ikiwa nitawahi kuwapo kwenye msimu wowote, ama wakati wowote kuwa bora zaidi kwa Bwana, pengine ingekuwa sasa hivi, unaona. Maana, mambo yote ya kitoto yamepita, nawe unatulia, unakuwa na mvi, na, unajua, ni wakati wa maisha tu ambapo kwa kweli unapaswa kuwa umetiwa nanga na una nguvu za kutosha bado, na kwa ubora wako kabisa; umetulia kabisa, sehemu ya utoto, na ujana umeondolewa, kwenye wakati tu wa kuingia hudumani. Na kama pengine nitawahi kujua chochote nilicho nacho, ninapaswa nikijue sasa. Nami ninashukuru sana kwa yale ambayo amenionyesha katika Injili Zake, na jinsi ninavyolifurahia sana jambo hilo.

33 Lakini mimi—mimi, bado, si—siwezi kujiridhisha, kwa namna fulani. Mimi—mimi tu, jambo fulani, ninamwonea Mungu njaa. Mimi…Kuna kitu ambacho ninapaswa kuwa nikifanya, inaonekana, na siwezi tu kukifanya vizuri, kwa njia fulani. Ninii…Ilikuwa hapa, miaka mingi iliyopita, nilikuwa nawaambia, ningeweza tu kunyoshea mkono kitu fulani na karibu kukigusa, unaona. Inaonekana kwangu kama kuna kitu kingine huko nje, ninakaribia kugusa mahali fulani. Laiti ningeweza kufika mahali hapo, na ninii…hiyo—hiyo itakuwa sawa.

34 Sasa, niliulizwa kuhusu kitabu ambacho Bw. Church aliandika, ama mambo yaliyomo mle ndani. Na, loo, wengi wamekuwa wakipiga simu, wakauliza kama ningesema lolote kuhusu jambo hilo, na kadhalika. Hapana, sisemi chochote kuhusu hilo. Naachana tu nalo, unaona.

35 Sikiliza, labda nitakuwa nikihubiri uponyaji wa Kiungu wakati Bw. Church atakapozikwa. Kwa hiyo sasa, unaona, uponyaji wa Kiungu…Wakati mimi na Bw. Church, sote wawili, tunalala kwenye makaburi yetu, Biblia ya Mungu bado itahubiriwa, ikifundisha uponyaji wa Kiungu, na watu watakuwa wanaifanyia kazi. Kwa hiyo, haileti tofauti yoyote. Hiyo ni…ni vibaya sana kwamba sisi wahubiri wa Kimarekani hatuna ya kutosha kufanya ila tu kwenda huku na huko na kubishana sisi kwa sisi, kujiokotea mzozo, kuchochea jambo fulani, unaona. Wakati, Neno la Mungu linatangaza uponyaji wa Kiungu. Na wamefanya jambo hilo, tangu nyakati kote kote, na daima itakuwa hivyo.

36 Na kuhusu kuamini kuwa Neno limevuviwa, ninaamini kwamba kila nukta katika Biblia hiyo imevuviwa. Hakuna hata kimoja Chake . . .

37 Acha nikupitishie tu jambo dogo hapa tunapoliwazia. Unajua ni nini huwafanya Waprotestanti wageuke Wakatoliki? Ni kwa sababu Wakatoliki wanaamini Neno hili limevuviwa. Mprotestanti anaamini baadhi ya sehemu Zake zimevuviwa. Sehemu anayotaka iwe imevuviwa, "Imevuviwa; mengine hayajavuviwa." Ikigusa mafundisho yake, "Haijavuviwa." Unaona, huyo ni Mprotestanti.

38 Mkatoliki anasema, kwamba, "Yote yamevuviwa, kila sehemu Yake, bali kanisa lao liko juu ya Neno. Kwa hiyo, haileti tofauti yoyote kile Neno lisemacho, ni kanisa." Kwa hiyo, singeweza kuwa Mkatoliki kwa hiari.

39 Sina chochote dhidi ya Wakatoliki. Ni marafiki zangu. Na kama wanamwamini Bwana Yesu Kristo, hao ni ndugu zangu, na kumkubali kama Mwokozi binafsi.

40 Sasa, makanisa ndiyo ninamaanisha. Ningeweza . . . Sikubaliani na fundisho la Kikatoliki. Nisingeweza kuwa Mkatoliki kwa njia hiyo, kanisa Katoliki la Kirumi, kwa sababu, wao, "Kutoweza kukosea kwa papa; na kanisa juu ya Neno; na kanisa kuwa juu ya Biblia." Nisingeweza kufanya hivyo.

41 Siwezi kuwa Mprotestanti kwa hiari, kwa maana siwezi kuchukua sehemu ya Neno na kusema, "Sehemu Yake imevuviwa, na sehemu *hii* imevuviwa; *hii* ilimaanisha kitu kingine, na *hii*."

42 Mimi ni mwabudu Biblia. Ninaamini kwamba hilo ni Neno la Mungu. Hakuna kitu juu Yake, kamwe hakutakuwa. Na mradi tu kuna Umilele, bado litakuwa ni Neno la Mungu. Unaona? Naamini ndivyo. Sasa, mimi . . .

43 Kunaweza kuwa na mambo ambayo sielewi. Labda mambo ambayo siwezi kuyatimiza, kwa imani yangu ndogo dhaifu niliyo nayo. Labda siwezi kulitimiza, lakini bado ni Kweli. Ni Neno la Mungu. Ni Neno la Mungu. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, ninaamini Hilo ni Neno la Mungu.

44 Nami naamini ya kwamba Humo ndani kuna—kuna Mbegu. *Hiki* ni kikapu kilichojaa Mbegu. Nami ninaamini ya kwamba Roho Mtakatifu huchukua Mbegu hiyo na kuipanda mioyoni mwetu, namna *hiyo*. Je, huamini hivyo? Nasi tunakuwa watoto Wake.

45 Kwa hiyo, basi, sina budi kuamini. Kama kuna Neno moja ambalo halijavuviwa, basi nisingeweza kukiamini Kitabu hicho. Nisingeweza kukiamini Hicho, maana, kama sehemu *Hii* haijavuviwa.

46 Bw. Church alisema, "Sehemu fulani za Biblia hazijavuviwa, kama vile Marko 16, na kadhalika." Anasema, "Haijavuviwa."

47 Mbona, nilikutana na marafiki zake wahudumu wa Methodisti, moja kwa moja huko New Albany, nao hawakukubaliana naye, kwa maili milioni mia moja. Walisema kwamba wao "hawangeweza kulivumilia hilo." Na mhubiri Mpresbiteri akisimama pale, alisema, "Naam, ndugu, si—sijui huyo mtu ana shida gani." Unaona? Sasa, alisema, "Naam, sasa tazama, yeye . . . "

48 Nikasema, "Hilo ndilo linalowafanya Wakatoliki. Hilo ndilo linalowafanya Waprotestanti walivyo, kundi dhaifu lisilo chochote." Unaona? Nikasema, "Hivyo ndivyo ilivyo, kwa sababu hawana matumaini yoyote. Hawawezi kujenga matumaini yao juu ya Biblia hii, maana, 'Sehemu Yake imevuviwa; sehemu Yake haijavuviwa.'"

49 Basi, si ajabu huyo Mwislamu . . . Dk. Reidhead, alipokuwa amesimama pale, na kumwuliza huyo Mwislamu kwa nini hakumkubali Bwana Yesu aliyefufuka. Akasema, "Vema," akasema, "ngoja niwaone nyinyi waalimu mkitimiza Neno lenu, yale ambayo Yesu wenu alisema lingefanya."

50 Akasema, "Loo, unarejelea Marko 16." Anasema, "Hilo halijavuviwa."

51 Akasema, "Unasoma Kitabu cha aina gani?" Akasema, "Korani yetu, kila sehemu ya Korani yetu imevuviwa." Hiyo ndiyo Biblia ya Mwislamu. Kasema, "Imevuviwa. Tunaamini kila neno lake. Na kila kitu ambacho Muhammed aliahidi, tunaweza kuifanya iseme hivyo." Hiyo ni kweli. Akasema, "Sasa nyinyi—nyinyi watu ifanyeni Biblia hii kusema hivyo." Kasema, "Sasa, kama haijavuviwa, basi hamna chochote." Unaona? Haya basi. Kasema, "Hamna kitu ila nadharia ndogo akilini mwenu." Naam, mtu huyo yuko sahihi kabisa. Awe mpagani, awe mpagani hapo; yuko sahihi kabisa.

52 Lakini ninasema imevuviwa, na kila Neno Lake ni Kweli. Kila Neno Lake ni Kweli.

53 Na hebu nikuonyeshe kitu. Yesu Kristo alisema, alipoandika sura ya mwisho katika Biblia hii, alisema, "Yeye atakayeongeza, ama kuondoa katika Neno hili, huyo ataondolewa katika Kitabu cha Uzima." Je, hiyo ni kweli? "Ambaye huongeza Kwake, au kuondoa Kwake."

54 Kwa hiyo naamini, kwa moyo wangu wote, kwamba kuanzia "Hapo mwanzo" wa Mwanzo, hadi "Amina" katika Ufunuo, imevuviwa na Mungu. Kila sehemu yake ni Ukweli. Hakuna Neno Lake hata moja lisilo sahihi. Yote ni Kweli. Ninaamini kila Neno Lake. Sitaki kuondoa, au kuongeza lolote. Sihitaji chochote zaidi; nahitaji Hilo tu. Na Hilo tu ndilo ninalohitaji.

55 Una maoni gani kuhusu hilo, Gene? Unafikiri hiyo karibu ni Kweli? Ninaamini ni Kweli, kila Neno Lake, kwa hiyo tunaliamini tu hivyo.

56 Sasa, ukipata watu wenye maono finyu, Marekani. Angalieni hapa, marafiki, ambapo tunabishana kuhusu kuwa Mmethodisti, au Mbaptisti, au Mpentekoste, na juu ya ushahidi, na mambo haya mengine yote. Maelfu mara maelfu, kila siku, wanakufa, ambao hawakuwahi kusikia habari za Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Takriban watu laki moja na arobaini elfu hufa kila siku, wasioongoka. Na tunabishana kama ni lazima unene kwa lugha, ama kama ni lazima upaze sauti, ama kama ni lazima uwe mfuasi wa Methodisti, ama Baptisti, ama kanisa la Kipentekoste, maskini vitu vya kale. Na sisi wahubiri, wavivu, tumelala hapa, tusifanye lolote, kote Marekani, tukiwahubiria watu ambao wamehubiriwa, tena na tena na tena. Ni kama kupekua, na kupekua, na kupekua. Ndivyo ilivyo. Na mamilioni katika nchi nyingine!

57 Naye Yesu, agizo la mwisho kabisa alilotoa, lilikuwa, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili hii kwa kila kiumbe." Je, unaweza kuona basi, rafiki, ni kwa nini siwezi kukaa nyumbani? Kuna kitu tu ndani yangu, kinachonirarua vipande vipande. Ni—ninatambua jambo fulani halina budi kufanywa, ndugu, dada. Sisi. . .Si—siwezi kulifanya, mimi mwenyewe. Na mimi—mimi sijui kile. . .

58 Ninaona jumuiya hizi za kimishenari, na jinsi zinavyojikunja na kushindwa, na chochote kile, kule, kwa sababu walipata jambo baya kwenda nalo. Huko, na theolojia. Vema, hao watu hucheka jambo hilo. Huwezi kwenda huko na theolojia. Hata hawaamini mambo hayo. Huna budi kuwaonyesha kwamba Mungu ni Mungu. Hiyo ni kweli.

59 Na mtu anaweza kufanya nini? Sijui. Lakini najua, moja ya siku hizi, yote yatakwisha, nayo tarumbeta ya Bwana italia, na kusema, "Hakutakuwa na wakati tena."

60 Ninawazia wakati Danieli alipokuwa amesimama pale ukingoni siku ile, naye akaona ono hilo. Ndipo Malaika akashuka, amevikwa jua, upinde wa mvua juu ya kichwa Chake. Akaweka moja, nchi kavu, alikuwa na mguu mmoja juu ya nchi, na mmoja juu ya bahari; akainua mkono Wake, akaapa kwa Yeye aliye hai hata milele na milele, ya kwamba, "Hakutakuwa na wakati tena." Unaona? Hum! Mimi—mimi. . .Hilo halina budi kutukia, moja ya siku hizi. Kila Neno Lake litakuwa kama vile Yeye alivyosema lilikuwa.

61 Kwa hiyo, basi, na kisha nitafanya nini basi? Utafanya nini basi? Unaona? Unawajibika, kama vile tu mimi ninavyowajibika. Sisi sote tunawajibika. Tunawajibika kwa kifo cha Yesu Kristo, kila mmoja wetu, mpaka tumkubali kama Mwokozi wa kibinafsi, kisha tumfanyie kazi kwa moyo wetu

wote. Ikiwa Mungu ametupa jambo la kufanya, tunashindwa kulifanya, basi Mungu atalihitaji hatimaye.

62 Loo! Kwa hiyo, Mungu, nipe imani, nipe—nipe ujasiri. Nitie moyo!

63 Ninakuwa rahisi sana kuvunjika moyo, unaona, kwa sababu naona mambo na ni makosa, na mimi—mimi siwezi kunyoosha. Hakuna haja ya mimi kujaribu kulinyoosha. Hakuna haja kabisa. Kama tu kubishana na huyo ndugu kuhusu kitabu chake. Hupati chochote kwa kubishana.

64 Hapa si muda mrefu uliopita, A. B. Neums . . . Unamjua; yule mtu aliyekufa wiki iliyopita. Alikuwa akinijia, akinihangaisha tu na kadhalika, kuhusu uponyaji wa Kiungu. Sasa, Ndugu Neums ni mtu mzuri; ninatumaini yuko Utukufu, leo, pamoja na watakatifu wengine wa Mungu, wakipiga kelele za ushindi.

65 Sasa, ni mtazamo gani aliochukua kuhusu uponyaji wa Kiungu, sijali kama kila mhubiri, papa, na chochote kile, kitainuka na kuhukumu uponyaji wa Kiungu, kesho nitakuwa nikihubiri uponyaji wa Kiungu. Hiyo ni kweli. Unaona? Kwa sababu gani? Iko katika Neno. Ni Neno la Mungu. Ni kile Mungu alisema. Siyo . . . Ninawajibikia yale ambayo Mungu alisema. Nami ninawajibika, kama mhudumu, kuhubiri kile Mungu alichosema, na kukiita Kitu hicho Kweli.

66 Nilikuwa nikienda kumchukua Ndugu Boze. Nikafungua redio. Ninapenda kumsikia Ndugu Neums; yeye ni mhubiri mzuri. Nami nikaenda kumsikiliza. Na akiwa njiani kule, loo, jamani, alikuwa akiukosoa uponyaji wa Kiungu, kuwa ni ushupavu wa dini, na mashetani na chochote kile. Naye akasema, "Kwa mfano, ndugu wa Bosworth." Akasema, "Nilipokuwa . . . wao . . . Nilikuwa nao walipokuwa katika ubora wao, walipokuwa vijana, wote wawili watoto tu." Ndipo akasema, "Wote wawili walikufa, wakiwa tu wavulana." Kasema, "Kama kungekuwa na jambo lolote la uponyaji wa Kiungu, vipi kuhusu hilo?"

Nikawazia, "Loo, Ndugu Neums! Jamani!"

67 Akasema, "Aimee McPherson alikufa, si chochote ila msichana, unaona, mtoto mdogo tu." Na Aimee alikuwa mwanamke mkongwe alipokufa.

68 Kwa hivyo nikawazia, "Loo, jamani." Vema, nikatoka, nikawazia, "Ninajua kwamba amefanya kosa kama hilo." Kwa hivyo nilitoka kwenda kwenye—kwenye—kwenye eneo la ndege huko, ndipo ni—nikaingia. Nikampigia simu. Nikasema, "Ndugu Neums?"

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Huyu ni Ndugu Branham."

Akasema, "Unataka nini?"

69 Nami nikasema, "Ndugu Neums, umefanya kosa kidogo asubuhi ya leo, ambalo litakuumiza, usipochunga, ndugu. Naamini ungenifanyia jambo lilo hilo. Lakini ulizungumza na kusema, 'Ndugu wa Bosworth walifariki wote wawili walipokuwa watoto wadogo.'"

Akasema, "Walifariki."

70 Nikasema, "Ndugu Neums, B. B. yuko Detroit sasa, akiwa na m—mkutano. Na F. F., Fred Bosworth, ndiye meneja wangu." Nami nikasema, "Anakaribia miaka themanini. Yeye yuko Miami, wakati huu." Tena nikasema, "Ndugu Neums, miaka miwili iliyopita, tulifanya uamsho papa hapa Louisville, pamoja, ambapo maelfu ya watu walikuja na kumsikiliza Ndugu Bosworth." Nami nikasema, "Picha yake inatoka kwa maelfu ya watu, kote nchini hapa, na kila kitu, makala zake na kadhalika." Nikasema, "Anaishi leo, na katika afya bora kabisa." Nikasema, "Mtu mwenye nguvu hapa, mwenye umri wa karibu miaka themanini, angali anahubiri Injili; amerudi tu kutoka Afrika, pamoja nami." Nikasema, "Huo ndio ukweli."

71 Nikasema, "Ndugu Neums," nikasema, "Naamini ungenifanyia jambo lile lile." Nikasema, "Naam, u—una ujumbe mkuu wa uamsho hapa kwenye redio, na kadhalika. Una. . . U—una nanii wote. . . na watu wengi wanakusikiliza. Na, Ndugu Neums, kama wakigundua. . . Na wanajua kwamba, maelfu ya watu wanakusikiliza, wanamjua Bosworth, sasa hivi." Nikasema, "Ukitoa tamshi kama hilo, litaumiza huduma yako, na sisi ni ndugu. Hupaswi kufanya hivyo."

Akasema, "Nitalinyoosha."

72 Sasa, unaona, hakuna haja ya kupigana. Mungu hushughulikia mambo yote, unaona. Usifanye hivyo. Upendo tu. Rudisheni wema kwa ubaya kila wakati. Je, hiyo ni kweli? Mtu yeyote anaposema mema juu yako; vizuri, shukuru. Ikiwa mtu yeyote anazungumza mabaya juu yako; wabariki hata hivyo. Hakika. Hiyo ni kweli. Hebu. . . Mungu hushughulikia mengine. Yeye Ndiye. Hiyo si ni kweli? Yeye Ndiye. Kwa hiyo, hata hivyo, sote hatuna budi kujibu Kwake.

73 Na haijalishi ni nini, ikiwa adui yako mkuu. . . Ikiwa una hisia yoyote, na adui mbaya zaidi uliye naye, ambaye unajua alikuwa anaenda mahali kama kuzimu, ingekufanya ujisikie vibaya.

74 Sijui mtu, sijui. . . siwezi kuwazia mtu wa chini kabisa duniani, leo, kwamba alikuwa Stalin kule juu, yeyote yule, ningechukia kujua kwamba mtu huyo alikuwa anateseka katika mateso ya kuzimu asubuhi ya leo. Ningechukia kujua hilo. Hakika ningechukia. Ninaomba Mungu airehemu nafsi yake iliyopotea, alipokuwa akifa, unaona, kwamba Mungu hatamwacha ateseke hivyo, . . . ?. . . Mwazie mwanadamu katika mateso ya kuzimu, ambayo Biblia inaonyesha hapa kwa

asiyeamini. Hebu wazia, mwanadamu, kwa nini, mimi... Ingefanya moyo wa jiwe kutaka mtu aende mahali kama hapo. Ningefanya kila niwezalo kumwepusha nako. Hakika ningefanya. Na nimwonee huruma, hadi ndani kabisa ya moyo wangu, kama angeenda mahali kama hapo.

75 Sasa, unaweza kuona ndugu akitenda mabaya, na—na kujaribu kumwelekeza, lakini ikiwa hatasikia, basi jambo pekee la kufanya ni kumpenda, kwa vyovyote vile, na kumwombea. Sivyo?

76 Sasa, ni wangapi wanampenda kwa moyo wako wote? Kwa moyo wako wote, mpende tu Bwana. Hiyo ni nzuri tu. Sasa dumisha hilo. Dumisha tu hilo. Na utake tu kumpenda Yeye zaidi.

77 Sasa, asubuhi ya leo, katika Neno la kale lililobarikiwa hapa! Loo, ni jambo la kustaajabisha sana kusoma hili—hili Agano Jipya, Agano la Kale, lolote la Hiyo. Lakini, mlango wa 4 wa Matendo, asubuhi ya leo, ambapo tunaanza kwa ajili ya onyesho dogo tangulizi sasa. Tunarudi nyuma. Huu ni wakati ambapo kanisa lilikuwa limeamshwa tu. Na huu ndio wakati ambao tunapenda kuzungumzia.

78 Sasa, mtu fulani, usiniruhusu nizungumze kwa muda mrefu sana. Nina ibada ya mazishi mara tu baada ya ibada hapa, katika Coots' Chapel, alasiri ya leo saa nane, ya Bw. Underwood. Na kesho alasiri, Bw. Tinsley, jirani yetu hapa, alikufa jana. Na kwa hivyo, umri wa miaka themanini na mitano, na kwa hivyo nina mazishi yake kesho.

79 Ndio kwanza nimwombe Dada Gertie kama angekuja na wimbo kwa ajili yangu, kucheza wimbo, maana sidhani hata wana wimbo ama chochote kile alasiri ya leo, watu, nadhani. Nami nitamwomba Dada Gertie kama angekuja kunichezea, alasiri ya leo. Labda tunaweza kujiandaa kwa ajili ya kesho, kwa ajili ya mazishi ya Bw. Tinsley.

80 Sasa, katika wakati wa mwanzo wa kanisa hapa, kundi hili la kwanza la watu, wote walikuwa...

81 Israeli walikuwa kidogo wamekanyagwa, kwa miaka na miaka, lakini sasa ilikuwa imefika mahali ambapo Masihi alikuwa amekuja na kuwapa tumaini, juu ya huyu Bwana Yesu. Lakini, mwanzo, aliteswa, alidhihakiwa, alitemewa mate, akaitwa "mtakatifu anayejifingirisha," kila kitu, au "shupavu tu, Beelzebuli, ibilisi," na kila kitu kingine. Lakini Yeye alikuwa na kusudi moja, na hilo lilikuwa ni kufanya mapenzi ya Mungu. Na haidhuru ni watu wangapi walikuwa wanampinga, bado Yeye alikuja kusudi Neno la Mungu lipate kutimizwa. Je, hiyo ni kweli? Unaona?

82 Sasa waangalie wasomi na walimu wa siku hizo. Mbona, walikuwa ni wasomi zaidi ya chochote ambacho tungeweza kuzalisha leo, kuhusu usomi. Na, kwa habari ya utakatifu,

mbona, wangelifanya kanisa la utakatifu leo kujionea aibu, linapofikia suala la utakatifu. Kwa kweli iliwabidi kuishi watakatifu. Waliishi maisha ya kujitenga, yaliyowekwa wakfu. Kama makasisi wa Katoliki ya Kirumi, siku hizi, si kama wao hata kidogo, maana wako nje katika parokia. Lakini hawa wote iliwabidi kuwa mahali pamoja, papo hapo hekaluni; maelfu mara maelfu yao mle, wametengwa, wamewekwa wakfu, kama tu vile Mji wa Vatikani.

83 Nao walikuwa ni wasomi wa Maandiko. Ilibidi wajue yote, herufi kwa herufi tu, kwa herufi. Nao walikuwa wakamilifu sana katika hilo, hata mpotoshaji katika andiko angeleta tofauti kubwa katika kila kitu. Iliwabidi "usiguse, usishike." Na hata kama walikuwa. . .Ilibidi wawe. . .Biblia ilisema, "Walipatikana bila lawama." Sasa, hiyo ni kuijua kweli, sivyo?

84 Hao wote, na, hata hivyo, wakiwa wameweka vichwa vyao kwa nguvu juu ya jambo moja thabiti walilofundishwa, na bila kuwa tayari kubadilika kwa Injili, Nguvu zote za Mungu, walishindwa kumtambua Bwana Yesu Kristo. Huyo hapo, na Maandiko yote yalinena juu ya kuja Kwake, lakini walishindwa kuitambua kwa sababu walikuwa na theolojia yao wenyewe. "Sisi ndio kanisa! Na ikiwa chochote kinakuja, huja kupitia sisi. Na tunatawala nchi na dini. Na sisi ni *hiki*, na sisi ni *kile*." Picha nzuri sana ya Ukatoliki leo. Unaona? "Tuna kila kitu chini ya hali yetu wenyewe."

85 Na ndipo wakagawanyika katika itikadi ndogondogo, kama vile Mafarisayo, Masadukayo, tofauti. Mafarisayo waliamini katika roho, na Malaika, ufufuo. Masadukayo hawakuamini Malaika, roho, wala ufufuo. Na wote walikuwa na namna yote ya—ya dhehebu tofauti miongoni mwao, kama tu tulivyo nao leo, jambo lile lile.

86 Na hapa palikuwa na mtu aliyeinuka, akasema, "Sisi ni mtu mkuu." Mmoja akainuka, kama Yesu, akawapeleka watu mia nne nyikani; wote wakaangamia. Ndipo wengine wakainuka, wakisema wao ni watu mashuhuri, na kuwaongoza kwenye aina fulani ya maskini dini potovu, na kadhalika.

87 Na moja kwa moja katikati ya wakati huo wote, kile kitu halisi, cha kweli cha Mungu kilikuja ulimwenguni; kitu halisi. Loo, jamani! Hiyo ingetufanya tufurahi mara moja. Alikuja, akiwa hana madhehebu, hakubaliani na madhehebu, hakubaliani na kanisa; bali akifanya jambo moja, mapenzi makamilifu ya Mungu yaliyoandikwa katika Biblia. Hiyo ni kweli. Alikuwa na Wake. . .Alijua kile ambacho Baba alisema. Alijua Maandiko, kwa uvuvio. Kwa hiyo alikaa, bila kujali walisema nini.

88 Alisema, "Mbona, enyi wanafiki!" Alisema, "Mnafanya mapokeo yenu kuwa ya kulazimisha sana, na kadhalika namna

hiyo. Na ninyi, kwa mapokeo yenu, mnalitangua Neno la Mungu." Unaona?

89 Loo, jinsi alivyoiweka kwenye mwamba wa kuchongea, kila sehemu yake, ndugu. Aliendelea moja kwa moja, hakuna kilichobadilika. Loo, napenda njia Yake isiyo na woga, nanyi je? Hakuna wakati ambapo Yeye aliwahi kufadhaika hata kidogo. Alijua alitembea kikamilifu katika mapenzi ya Mungu.

90 Wakati dhoruba zinavuma, maskini mashua ya kale ikiwa karibu kuzama; alijitokeza akitembea ametulia tu kadri alivyoweza, akaweka mguu Wake juu ya demani ya mashua. Akatazama juu, akasema, "Amani," kwa Baba, "Amani." Akatazama juu ya bahari, akasema, "Tulia." Akarudi nyuma na kujilaza. Mawimbi yalitulia kabisa. Huyo alikuwa ni Yeye. Hana woga. Hajasisimkwa. Hana ugomvi.

91 Walisema, "Loo, tunajua Yeye ni nani, Beelzebuli. Tunajua anafanya haya kwa nguvu ya mkuu wa mashetani."

92 Akasema, "Ikiwa Shetani anamfukuza Shetani, basi ufalme wake umegawanyika. Na ikiwa mimi, natoa pepo kwa kidole cha Mungu, watoto wenu huwatoa kwa nani? Iweni waamuzi." Kwa utulivu tu kadiri awezavyo kuwa. Kamwe . . . Mbona, imani ilikuwa tu fahamu ndogo Kwake. Yeye aliendelea tu kutembea, maana alijua alikuwa anafanya mapenzi ya Mungu kikamilifu.

93 Alipowaponya wagonjwa, Biblia ilisema nini, sababu ya Yeye kuwaponya wagonjwa? "Aliwaponya wagonjwa, ili jambo hilo litimie." Kwa nini? Unaona? Kwa nini? Ni rahisi kuamini chochote anachosema Mungu.

94 Mungu akisema, "Kesho, kwamba, kutakuwa na joto sana, kwamba kila mtu anaweza kwenda kuogelea," haitakuwa vigumu kwangu kuweka tayari suti ya kuogelea. Kama akisema, "Mvua itanyesha kesho, mchana kutwa," ni rahisi kwangu kubeba mwavuli. Je, hiyo ni kweli? Mungu akisema, "Itakuwa msimu mzuri mwaka ujao, kwamba mazao yote yatakua, kila mahali," ninaweza tu kupanda chochote, kwa nia njema. Unaona? Je, hiyo ni kweli? Mungu akisema atatupa mkutano mkuu usiku wa leo; ni—ningekuja bila hata fungu akilini mwangu. Atafanya hivyo, kwa vyovyote vile. Je, hiyo ni kweli? Mungu amesema hivyo! Hilo latosha.

95 Kama unaugua, karibu tu kufa, na Mungu akasema, "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Hilo halikutikisi hata kidogo; endelea tu. Mungu alisema hivyo! Unaona? Hiyo ni imani tu isiyo na fahamu, kitu kama hicho, unaona. Endelea tu moja kwa moja, ukiamini. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha tu.

96 Vema, ilikuwa rahisi kwa Yesu, kwa sababu alijua Yeye "alikuja katika mwaka uliokubalika," kufanya jambo la Mungu, na kuhubiri Neno la Mungu, na kufanya ishara za Mungu, na kutimiza yale ambayo Mungu alisema yangekuja kutimia. Vema,

kwa nini kanisa, leo hii, lisiwaze jambo lile lile, Maneno yale yale ambayo Yesu alisema! Unaona?

97 Maana, sisi, wengine, tunarudi nyuma na kusema, “Loo, siku za miujiza zimepita. Utukufu kwa Mungu. Sehemu *Hii* haijavuviwa. *Hiyo* imevuviwa, lakini *Hii* haijavuviwa, kwa sababu mambo hayo hayawezi kutokea leo.” Unaona? Hiyo ndiyo sababu hatuwezi kusonga.

98 Loo, kama Mwili mmoja mkuu wa Kristo utainuka katika upendo, na heshima, unaona, na kuendelea moja kwa moja, kama moyo mmoja katika nia moja, bila fahamu ya imani iliyo karibu nao! Ndugu, ungeona kanisa duniani ambalo lingeninii . . . Ule Utawala wa Miaka Elfu ungeingia papo hapo. Ni kuja. Ni kuja. Loo, ndiyo. Na kwa neema ya Mungu tutaiona. Nitakuwa papo hapo. Hiyo ni kweli. Mungu ameahidi. Ninamwamini, kwa hiyo nitakuwa papo hapo itakapotukia.

99 Sasa, sasa, ilivunja mioyo ya wanafunzi walipojua Yeye alikuwa anaondoka. Alisema, “Nitaondoka. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona Mimi tena,” alisema.

100 Walisema, “Anazungumza nini? Yeye ndiye Mtu mgumu kuliko wote kuelewa.” Hakuna aliyemwelewa. Mbona, wangesema . . . Akawaambia ndugu Zake . . .

Ndugu zake wakasema, “Twendeni kwenye sikukuu.”

Akasema, “Siendi huko.”

101 Walipoondoka, alisema, “Ninaenda njia nyingine. Siendi nao.” Maana, ndugu Zake hata hawakumwamini. Hiyo ni kweli. Watu wake mwenyewe hawakumwamini. Alisema, “Ninaenda njia nyingine.” Mbona, walishangaa ni vipi.

102 Naye akasema, “Mtu huyu anaongea kwa mafumbo. Hatuwezi kuelewa.”

103 Huku hapa katika mlango wa 17, alisema, “Tazama . . . ” Kabla tu hajaenda Zake Utukufuni, alisema, “Tazama, sasa wanena waziwazi, na si kwa mafumbo, wala kwa methali, na kadhalika.”

104 Unaona, wangesema, “Sasa Yeye alisema *hivi*?” Nikodemo, alipokuwa akizungumza Naye, alisema, “Mtu anawezaje kuzaliwa mara ya pili?” Akasema, “‘Mtu asipozaliwa kwa maji,’ mambo haya yote, inawezekanaje?” Hawangeweza kuelewa. Alisema, “Mtu huyo anazungumza kwa mafumbo.” Hakuna mtu aliyeielewa. Hata mama Yake mwenyewe hakumwelewa.

105 Alikuwa ni Mtu mgumu kumwelewa, kwa maana Yeye alikuwa wa Mungu, na akili zao zilikuwa za ulimwengu. Kwa hiyo, Yeye aliifanya kuwa tofauti kabisa, basi. Akili ya ulimwengu dhidi ya u—u—uvuvio wa Mungu, mbona, ni upumbavu. Lakini jambo la ajabu, kwamba Yeye alikuwa na uwezo wa kufanya yale aliyosema angefanya. Hapo ndipo

ilipofikia. Naye angeweza kufanya mambo ambayo watu wengine hawangeweza kufanya.

106 Hivyo basi akasema, "Sasa kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, lakini ninyi mtaniona." Sasa sikiliza hili, "Lakini ninyi mtaniona." Hiyo "ninyi," alikuwa anazungumza na nani? Waumini. Je, hiyo ni kweli? Alisema, "Mtaniona Mimi. Kwa kuwa Mimi," sio mtu mwingine, "kwa maana Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, ili . . . " "Mwisho wa mitume"? [Hapana.] Kwa muda gani? " . . . ukamilifu wa dahari." Kote kote, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele."

107 Sasa, "Ninaondoka. Nitamwomba Baba; Yeye atawapa mfariji mwingine, ambaye ni Roho Mtakatifu." "Mimi," kiwakilishi cha nafsi, ambacho kilikuwa mwili. "Mimi ninaondoka. Namwomba Baba, kabla sijaenda; Baba yu ndani Yangu. Naye atawatumia mfariji mwingine, ambaye ni Roho Mtakatifu. Yuko ndani Yangu sasa. Atakapokuja, ataukemea ulimwengu kuhusu dhambi. Na mambo yale yale nifanyayo, mtayafanya. Sasa, ninawatakeni mwende ulimwenguni mwote na kuhubiri Injili kwa kila kiumbe."

108 Injili ni dhihirisho la Nguvu za Mungu. Unaona? Yule ambaye Inj- . . . Paulo alisema, "Injili haiji kwa maneno tu, bali kupitia nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu."

109 "Sasa enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri injili. Tazama, niko pamoja nanyi siku zote, hata . . . " "Hadi mwisho wa mitume"? Hapana. Namaanisha, " . . . mpaka ukamilifu—ukamilifu wa dahari." "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena. Watalikosoa, walidhihaki, kama tu wanavyofanya sasa," akasema. "Bali ninyi, muumini, mtaniona; kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Ningependa kuona mtu akisugua na kuondoa hilo? "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele." "Mambo yale yale nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya."

110 Sasa hiyo ama ni kweli au si kweli. Na kama ni kweli, Italifanya kweli. Na ninaweza kulithibitisha, papa hapa, asubuhi ya leo, kwamba ni kweli, kwa neema ya Mungu, akifanya mambo yale yale aliyofanya wakati huo.

111 Sasa ulimwengu unasimama na kusema, "Aha, Mtu huyo amerukwa na akili. Ana kichaa. Hiyo si kitu. Hao watu wamesisimkwa tu." Unaona? Maana, hiyo ndiyo dunia. Lo, unaweza kuwa na jina kubwa, lakini hilo halina uhusiano wowote nalo. Vipi kuhusu *Huko* juu? Unaona? Sawa. Sasa, tunaamini kuwa ni vivyo hivyo.

112 Ndipo, wanafunzi, walistaajabu. Wakasema, "Ee Bwana, unakwenda wapi? Loo, mimi—mimi . . . Wapi, unaenda wapi, nasi hatuwezi kwenda pamoja Nawe?"

113 Na mlango huu wa 14 wa Yohana Mtakatifu, Yeye aliifafanua. Alisema, "Ninaenda nyumbani kwa Baba Yangu,

kwa maana Huko ndani kuna makao mengi. Nitaenda na kuwaandalia mahali. Nitakuja tena kuwachukua, siku moja, niwakaribishe Kwangu; ili nilipo, nanyi pia mwepo." Na—na Yeye akasema, "Mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya."

114 Tomaso akamtazama, ama Filipo, hasa, na kusema, "Bwana, tuonyeshe Baba. Ni nani—ni nani huyu Baba unayeenda kwake?"

115 Akasema, "Mbona, nimekuwa na wewe kwa muda mrefu. Hunijui Mimi?" Akasema, "Mnaponiona Mimi, mmemwona Baba. Baba yu ndani Yangu. Amini kwamba mimi na Baba tu mmoja. Au, niaminini Mimi kwa ajili ya kazi iyo hiyo, ya kwamba Baba yu ndani Yangu. Si Mimi nizifanyaye kazi hizo; ni Baba aliye ndani Yangu, afanyaye kazi."

116 Mimi si Roho Mtakatifu. Wewe si Roho Mtakatifu. Lakini ikiwa kuna chochote. . . *Yeye* si Roho Mtakatifu. Lakini jumbe hizo anazohubiri hazikuwa zake. Ni Roho Mtakatifu ndani yake. Je, hiyo ni kweli? Vema, baadhi ya siku hizi, sura yake hii yote, ndogo, ya kizamani itaanguka chini, lakini Roho wake Mtakatifu na roho yake huwa kitu kimoja. Na Roho Mtakatifu alipomfufua Yesu kutoka kaburini, pia anauleta mwili wake katika ufufuo, unaona. Kwa hivyo hayo ndiyo matumaini tuliyo nayo leo.

117 Kwa hiyo, vema, wote walivunjika moyo, nao wakapanda, kwenye Siku ya Pentekoste. Naye Yesu akawaambia, akasema, "Nenda huko na usubiri."

118 Walimwona baada ya kufufuka Kwake. Walifikiri, "Loo, jamani, hii ni ajabu! Tunamwona ameinuliwa." Hata Tomaso akasema, "Bwana, mimi—mimi . . . "

119 Aliwaambia mitume, kwanza, "Hata sitaamini, isipokuwa naweza kuweka mkono wangu katika ninii Wake—ubavuni Mwake."

120 Na yapata wakati huo, Yesu akatokea chumbani. Akasema, "Tomaso," kasema, "njoo hapa." Akasema, "Gusa mikono Yangu. Weka mkono wako hapa ubavuni Mwangu." Akasema, "Niguse Mimi. Je, roho ina nyama na mifupa kama nilivyo nayo?" Kasema, "Mna chochote cha kula?"

Wakasema, "Ndiyo, tuna mkate na samaki, hapa."

121 Akasema, "Nipe baadhi yake." Naye akasimama pale na kukila, na kumeza. Akasema, "Sasa, je, roho inakula jinsi unavyoniona Mimi ninakula?"

122 Tomaso akasema, "Loo, si Bwana wangu tu, bali Yeye ni Mungu wangu." Akasema, "Bwana wangu na Mungu wangu!"

123 Akasema, "Sasa, Tomaso, kwa sababu umenigusa, na umeniona, nawe umenishika Mimi, na kila kitu, unaamini." Akasema, "Ni bora kiasi gani imani yao ambao hawajawahi kuniona na bado wananiamini Mimi." Unaona?

124 Akasema, “Sasa njoo huku nje.” Akatoka nje. Akasema, “Sasa, tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba.” Akasema, “Bali ngojeni katika mji wa Yerusalemu, hata mvikwe Nguvu zitokazo Juu.”

125 Akasema, “Sasa nataka ninyi mwende ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili; ulimwengu wote, na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Je, hiyo ni kweli? Akasema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; watakunywa vitu vya kufisha; wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Na alipofanya hivyo, Yeye—Yeye aliwapa agizo lao la mwisho.

126 Ni agizo gani la kwanza alilopata kuwapa mitume Wake? Mnataka niwasomee? Inapatikana katika—katika mlango wa 10 wa Mathayo. Yesu aliwaagiza wanafunzi Wake. Akasema, “Tokeni, pozeni wagonjwa, takaseni wenye ukoma, fufueni wafu, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure.” Mathayo mlango wa 10. Je, hiyo ni kweli? Hilo ndilo agizo Lake la kwanza kwa mitume Wake.

Agizo lake la mwisho kwa mitume . . .

127 Hao hawakuwa mitume tu, sasa. Walichagua sabini. Hiyo ni kweli? Sabini walikuwa wamechaguliwa. Naye akawapa wote sabini, akawatuma wawili wawili, wawili wawili. Alisema, “Pozeni wagonjwa, takaseni wenye ukoma, fufueni wafu, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure. Usichukue pesa, na nguo nyingi za kubadilisha, na sanduku kubwa, lakini vua tu.” Akasema, “Kwa maana mfanyakazi anastahili ujira wake. Usimfunge kinywa ng’ombe anayepura nafaka.” Akasema, “Endelea.” Ndipo wakatoka na kuhubiri. Hilo lilikuwa ni agizo Lake la kwanza.

128 Kisha, agizo Lake la mwisho lilikuwa, “Enendeni ulimwenguni kote . . . ” Sasa, kama agizo Lake la kwanza lilikuwa “kuponya wagonjwa na kutoa pepo,” utajaribuje kukatilia mbali agizo la mwisho, ambalo ni muhimu zaidi kuliko agizo la kwanza? Agizo la kwanza lilitolewa kabla Yesu hajatukuzwa, kabla ya Upatanisho kuwahi kufanywa. Na kama uponyaji wa Kiungu ulikuwa ni upande wa pili wa Upatanisho, na Upatanisho ukinena juu ya uponyaji wa Kiungu, tunawezaje kuukana upande huu wa Upatanisho? Hatuwezi kuukana. Hatuwezi kuukana. Sio tu ya kukataliwa. Ni Neno la Mungu.

129 Na kila wakati, kupitia uamsho wowote, wakati wowote ambao walipata kuwa na uamsho, walikuwa na uponyaji wa Kiungu na miujiza ndani yake. Kupitia kwa Moody, kupitia kwa Sankey, kupitia kwa Wesley, kupitia kwa Knox, kupitia kwa Calvin, wote, kila mmoja alikuwa na ishara na maajabu. Lakini ulimwengu umepoa, unaona. Ulipozwa basi, pia. Lakini walianzisha uamsho. Mwangalie John Wesley. Nena kuhusu miujiza! Martin Luther!

130 Hata watu wakuu, kama vile marais, kama Abraham Lincoln, George Washington, wote hao! Kabla ya Valley Forge, George Washington aliomba mpaka ubavu wake ukalowa, mpaka *hapa* juu, akiwa amesimama kwenye theluji. Siku iliyofuata, goboli—risasi tatu za goboli zilipita kwenye koti lake na hazikumgusa kamwe. Unaona?

131 Mbona, imekuwa miujiza wakati wote, naam, bwana, wakati wote. Mungu ni mtenda miujiza. Na wote wanaomwamini, waliozaliwa na Yeye, wana nia ile ile iliyokuwa ndani ya Mungu; iko ndani ya mtu huyo, kwa maana yeye ni mwana wa Mungu. Na hawezi kufanya lolote lingine ila kumwamini yule mkuu na mwenye uwezo, wa Kimbinguni, kwa sababu yeye ni sehemu ya huyo wa Kimbinguni.

132 Mwangalie Mungu, kabla hata hakujawa na chembe angani, kabla hakujawa na chochote, na hakuna chochote ila Mungu kila mahali. Alijaza nafasi zote na wakati wote. Akasema, "Na iwe," na ikawa. Ulimwengu huu tunaoishi, ni moja tu ya Maneno ya Mungu yanayozungumza na kujidhihirisha. Sasa, kama wewe ni sehemu Yake, huna budi kuamini jambo hilo. Lakini kama huliamini, inaonyesha hujawahi kuwa sehemu Yake.

133 Sikiliza. Sio yeye anayetaka kuokolewa, anayeokolewa. Ni yeye ambaye ameokolewa kwa chaguo la Mungu. Esau alitaka kuokolewa, pia. Alilia kwa uchungu, na hangeweza kupata mahali pa kutubu. Alitaka kuokolewa. Sio kwa sababu unataka kuokolewa. Mungu alisema, "Nimemfanya mgumu yule nitakayemfanya mgumu. Ninamhurumia nitakayemhurumia." Hiyo ni kweli. Alisema, "Kabla Esau au Yakobo, yeyote, kuzaliwa, bila kujua mema na mabaya," Mungu alisema, "Ninampenda Yakobo na ninamchukia Esau." Naye Esau alijaribu kujiweka sawa na Mungu, na asingeweza. Farao alijaribu kuwa sawa na Mungu, na asingeweza kufanya hivyo. Kwa hivyo, si wewe, si kile unachotaka. Ni kile ambacho Mungu amekukusudia kufanya. Hiyo ni kweli.

134 Paulo alisema, katika mlango wa 9 wa Warumi pale, "Hivi mfinyanzi hana mamlaka juu ya udongo, kufanya chombo cha heshima au chombo kisicho na heshima, ili kuonyesha utukufu Wake kwa wale aliowaheshimu?" Hukujua hilo, sivyo? Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema.

135 Farao alijaribu awezavyo kutubu. Alikuwa mwema. Alisema, "Hakika, nitawaacha mwende. Endelea."

136 Mungu alisema, "Hapana, huendi. Nitaufanya moyo wake kuwa mgumu ili usiweze kufanya hivyo." Maana, Neno la Mungu halina budi kutimizwa. [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake—Mh.]

137 Na kama tunaishi katika siku hii, wakati taratibu na mambo mengine yamelivunja kanisa, likasambaratika; mbona, ni Neno la Mungu likitimizwa. Hakika kama Mungu alivyosema,

"Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio;" kwa hakika kama vile Mungu alivyosema makanisa haya yatakuwa kama yalivyo sasa, Mungu pia alisema upinzani huu ungekutana nayo. Kwa hiyo, Mungu yeye yule aliyeweka ishara na maajabu, aliamuru kwamba hawa wanapaswa kuwatesa. Basi ndivyo hivyo. Ikiwa uko upande mwingine, ninasikitika. Nami nataka usiwe hivyo, lakini labda huwezi kujizuia. Unaona? Mungu anaweza kuwa aliitengeneza hivyo.

138 Niliwauliza, muda mfupi uliopita, kabla sijasema hivi, ni wangapi wenu mnampenda Bwana? Na kujua, ninyi nyote mlikuwa Wakristo, kwanza kabisa. Unaona? Maana, huwezi kuwa Mkristo . . . Hii sio ya nje, ulimwengu. Hii ni kwa ajili ya watu wa Bwana.

139 Huwezi kuwa Mkristo, isipokuwa Mungu amekuchagua. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote wanaokuja, ndipo nitampa Uzima wa milele, na kumfufua katika siku ya mwisho." Mungu alilikusudia tangu zamani, alilijua kimbele. Kabla ulimwengu haujaanza, Alisema alituchagua kimbele ndani ya Kristo, kama wana wa Mungu—wa Mungu, kabla ulimwengu haujaanza. Hatuna budi kuwa.

140 Na kwa sababu umegeuza mgongo wako, na ukawaona watu ambao wamezungumza nao; hawangeweza kulisikiliza. Wanaliinulia pua zao. Huku, labda wahudumu, labda wahubiri wa Injili, labda kile ambacho ungefikiria ni Wakristo mashuhuri, lakini hata hawajaokolewa. Hiyo ni kweli. Hata hawajaokolewa.

141 Waangalie hao Mafarisayo kule nyuma, wa kidini tu, na wachamungu, na safi, na watakatifu wawezavyo kuwa, na watu wenye nia ya Maandiko namna hiyo. Na Yesu akasema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi." Unaona?

142 Kuna mambo katika Biblia ambayo kanisa halijui lolote kuyahusu, rafiki. Kweli. Unaona? Na unashangaa wakati mwingine, jinsi mambo haya, "Mbona Biblia inasema hivi? Kwa nini Yesu akasema . . .?"

143 Petro alisema, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Na hapa tuna watu madhabahuni, wanaongojea *hili* na kungojea *lile*, wakati huo ungelitangua Neno la Mungu. Mungu hana budi kutunza Neno Lake. Na dakika ile unapotimiza masharti Yake, Mungu atalijibu Neno Lake upesi *hivyo*. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Sawa. Maana, Yeye yuko pale kuingojea.

144 Lakini unaona watu wakisema, "Loo, tusipopaza sauti, au tusiponena kwa lugha, isipokuwa tucheze katika Roho." Mambo hayo yote ni sawa. Yote ni sawa, lakini hayana uhusiano wowote na wokovu; hata kidogo.

145 Maana, mara tu unapotubu dhambi zako, kama kweli Mungu amekushawishi, na umetubu na kubatizwa katika Jina la Yesu

Kristo, Mungu anawajibika kukupa Roho Mtakatifu papo hapo, kweli, maana Neno Lake lilisema hivyo. Na Yeye hawezi . . .

146 Si kitu kwa upande wa Mungu. Ni sehemu yako, kwa sababu watu wamefundishwa visivyo. Kila wanapokuja, wanaanzisha kitu kidogo, wanasema, "*Hii* Ndiyo. *Hii* Ndiyo." Loo, jamani! Sio maonyesho haya ya kimwili; ni sifa za Roho Mtakatifu.

147 Lakini, kumpokea Roho Mtakatifu, ni kumpokea Mtu, Kristo, ndipo mambo haya mengine yanatukia maishani.

148 Tumeona watu wakipaza sauti, na kuishi kila namna ya maisha. Tumewaona watu wakinena kwa lugha, na kufanya vivyo hivyo. Tumewaona watu wakitoka na kuwaombea wagonjwa, nao wangeponywa; na kufanya, kuishi namna yoyote ya maisha. Yesu alisema, "Wengi watakuja Kwangu na kusema, 'Bwana, sikutabiri katika Jina Lako, nikahubiri? Je, sikutoa pepo kwa Jina Lako?' 'Ndiyo.' 'Je, sikufanya matendo haya makuu?' 'Ndiyo.' Atasema, 'Vema, basi, ondokeni Kwangu, ninyi watenda maovu. Hata sikuwajua.'"

149 "Si yeye atakaye, au yeye apigaye mbio, ni Mungu aliyerehemu," Biblia ilisema. Alisema, "Je, sikumwambia Musa, 'Ninamrehemu nitakayemrehemu, na ninamfanya mgumu nitakayemfanya mgumu'?" Paulo alisema, "Hakuna mtu . . . Vema, unasema basi, 'Anawezaje kuona kosa? Ikiwa Yeye alikuchagua tangu awali kwa uharibifu wa Milele, anawezaje kuona kosa?'" Akasema, "Loo, mwanadamu, je, kitu kilichoumbwa kinaweza kumwambia Yeye anayemwumba hivyo? Hawezi."

150 Kwa hiyo unaona watu ambao huwezi kuzungumza nao, na kamwe hawatasikiliza; nao hawatasikiliza Maandiko, huku wakiamini nusu Yake ni kweli na nusu Yake ni makosa, na hata hivyo wanafanya *hivi*.

Unasema, "Je, hao wanaweza kuwa wahudumu?"

151 Biblia ilisema hivyo. Ilisema, "Watu wa kale, walichaguliwa kimbele kwa hukumu hii, kuchukua neema ya Mungu na kuigeuza kuwa ufisadi." Ufisadi ni nini? Kujua Ukweli na usitembee ndani Yake!

152 Ilisema, "Wakati Kweli imewasilishwa kwa mtu fulani, aikatae makusudi, aipuuze; hakuna tena Dhabihu kwa ajili ya dhambi, iliyobaki kwa ajili ya mtu huyo." Kwa nini? Hakuna kitu ndani yake, kuamini. Unaelewa ninachomaanisha?

153 Tazama hapa. Unawezaje kulisha mwana-kondoo, uchafu? Asingeula. Hiyo ni kweli. Asingeula, kwa sababu yeye ni mwana-kondoo. Lakini nguruwe atakula. Unaona ninachomaanisha? Kwa sababu, yeye ni nguruwe, kwa asili.

154 Na wote waliokusudiwa Uzima wa milele, wataisikia Kweli na kuiamini Kweli, na kuja kwenye Kweli. Lakini wale ambao wataenda kanisani na kuwa wa kidini kama wengine

wao, hata hivyo hawataipokea Kweli, kwa maana hamna kitu ndani yao cha kuunganishwa Nayo. Hawawezi kuamini Mambo ya Kimbinguni, kwa maana hakuna ya Kimbinguni humu kuchanganyikana na ya Kimbinguni. Haya basi. Unaona ninachomaanisha? Hakuna kitu cha kimbi-. . .

155 Ninamwona mama fulani akiwa na mtoto mchanga mgonjwa amelala pale asubuhi ya leo. Nilimwona akishuka kwenye gari, nilipovuka barabara. Kitu, labda alisikia matangazo ya redio au kitu fulani. Alijua tulikuwa tunaenda kuwaombea wagonjwa. Kitu moyoni mwake kinasema, "Mpeleke mtoto huyo kanisani." Alitii hilo. Hiyo ni kweli, unaona.

156 Kwa maana kuna kitu humo ndani, kinasema, "Ni kweli." Unaona ninachomaanisha? Kilitoka wapi?

157 Kila wazo, kila kitu ulicho nacho, kinatoka mahali fulani. Hakina budi kuwa na mwanzo. Je, hiyo ni kweli? Loo, jamani! Ninapenda hili. Hakina budi kuwa na mwanzo. Na kwa hivyo asili hiyo ilianzia wapi? Unaona? Ilianza Utukufuni, ikazunguka katika ulimwengu wa Malaika. Wajumbe wa Mwenyezi Mungu wamefagia kote, wakasema, "*Hii* Ndiyo." Aliangalia Neno. Ilitoka wapi? Kutoka *Hapo*.

158 Na Huko, sehemu hiyo *Huko* juu, iko *hapa* ndani pia, inasema, "Ni kweli!".

159 Ni kama nikitaka kupiga simu California. Jambo la kwanza, ningeshusha kipokezi changu, nimpigie opereta. "Kituo kikuu?"

"Naam."

160 "Nipigie *Fulani-fulani*, huko California." Lazima nipitie kituo kikuu. Unaona ninachomaanisha? Kutoka nyumbani kwangu, hadi kituo kikuu; kutoka kituo kikuu, nchini kote. Ndivyo ilivyo.

161 "Lolote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, nitalifanya." Jambo la kwanza unajua, tunapaswa kupitia Kituo kikuu. Jambo la kwanza, unapaswa kupigia Kurasa, ili kuona kama kuna mahali kama hapo. Je, hiyo ni kweli? Na unapata mahali hapo, kisha unashuka na kusema,"Baba!"

"Naam?"

"Katika Jina la Yesu, nipe *hili*." Hiyo hapo.

162 "Bila shaka, Mwanangu! Chomeka ndani." Kipapasi kilirudi kikizunguka kwenye mstari, Neno la Mungu likidhihirishwa. Hakika, ndivyo hivyo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyo rahisi, ndivyo waaminio walivyo, ndivyo wokovu ulivyo, ndivyo uponyaji ulivyo. Kila kitu ambacho Mungu aliahidi kipo Hapo. Ni chako. Omba tu. Chochote alichokufa kwa ajili yake, ni chako.

163 Hicho hapo, kitu chote, na jinsi tunavyokipenda! Si ni chakula kwa nafsi yako? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na kila wakati tunapoamini, hiyo sehemu ndogo hapo ndani

inakuwa kubwa, kubwa zaidi, kubwa zaidi, inavimba, mpaka, baada ya kitambo kidogo, inakuwa tu, unaamini mambo yote. Na vitu vyote vinapoanza kuingia, upendo unaanza, unaingia; shaka, chuki, uovu, woga, hutoweka tu, namna *hiyo*. Inaenea tu, inakuwa kubwa sana, mpaka inapasua maskini hilo ganda dogo. Unaona ninachomaanisha? Ulimwengu wote unasafishwa. Tunakua kila siku katika neema ya Mungu.

164 Sasa unaona watu hao, wanaweza kuketi na kusema, "Vema, namkubali Bwana." Unachukua neno lao kwa ajili yake. Ningechukua, pia. Siwezi kuhukumu. Mungu huhukumu. Lakini katika miaka kumi kuanzia sasa, hawajawahi kuendelea hata kidogo; kukaa tu moja kwa moja mahali pale pa zamani. Unaona?

165 Tunakua kila siku. Kila siku moyo wetu una njaa, unazidi kusonga mbele. Kuna kitu kinakua ndani yako. Amina. Unakuwa mkubwa zaidi, unaenea, unaweza kuchukua ninii zaidi . . . ? . . . Paulo alisema, "Wakati wewe . . . " Aliliambia kanisa la Korintho, kasema, "Unakomaa, unakua. Lakini wakati mnapaswa kuwa walimu, mngali ni watoto wachanga wanaohitaji kufundishwa." Hiyo ni kweli? Wakati, mnapaswa kuwa walimu; Kitu mle ndani, kikikua, kikisukuma nje, kikizidi kuwa kikubwa. Roho Mtakatifu, akikua.

166 Kuzaliwa upya! Ikiwa kuzaliwa kumezaliwa kutoka nje, kutoka ndani kwenda nje, mtoto, hukua akiwa hai. Ikiwa sivyo, inabaki. Je, hiyo ni kweli? Naam, wakati Kuzaliwa kukiwa ndani, si kunapaswa kukua? Kristo moyoni mwako anapaswa kukua kila siku, kuwa mkubwa zaidi, mwenye nguvu zaidi, anaelewa mambo vizuri zaidi, kusamehe, kutembea kama vile Mungu angetembea, "hata Kristo aumbike ndani yako, tumaini la Utukufu."

167 Ni lazima tuwavumilie wanyonge hadi watakapokomaa kikamilifu katika Kristo Yesu. Ndipo wao ni askari wazuri. Ndipo wamevaa silaha kamili. Ukinena juu yao; haiwaumizi. Wacheke, wadhihaki; hawazingatii jambo hilo. Wanalo jambo moja; wao ni wakubwa sana, jamani, wamejaa Utukufu sana. Jambo pekee unalopaswa kuacha ni vazi hili kuukuu la mwili, na uendelee tu moja kwa moja hadi Utukufuni. Unaona?

168 Mtu anasema, "Unajua, mtu fulani alisema wewe ni mnafiki, Bibi Jones?"

"Kweli? Vema, Mungu awabariki."

169 "Je, unajua mambo fulani-fulani yanaendelea kwenye kanisa hilo, hayapaswi kuwa yanafanyika?"

"Vema, nitaliombea." Unaona? Mkubwa!

170 Loo, ikiwa wewe ni mdogo, basi unasema, "Loo, ni hivyo? Acha niingie. Nijiunge na upande gani? Unaona? Hapo ndipo unapopata shida. Hapo ndipo huwezi kukomaa.

171 Lakini unapokuwa mkubwa vya kutosha, mpana vya kutosha, unaona, umenenepa. Si tu kunenepa, lakini umekua. Kristo akikua ndani yako, akikua na kuondoa uovu, akiuondoa kutoka kwako; anausukuma nje. Mungu anapoingia, anausukuma tu nje. Unasema, "Loo, ni mdogo jinsi gani, ni mchanga jinsi gani, ni *watoto* jinsi gani, kubishana na kuzozana." Lakini, jambo la kwanza unajua, Hiyo inakulia tu juu yake. Hatuna nafasi tena kwa hilo. "Loo, nilikuwa ninachukia kuona *hili*, na kuchukia *lile*. Lakini, unajua, nimefikia tu ambapo silizingatii tena." Unakua. Naam, bwana.

172 Unajua, unapokuwa mchanga, wanadai kuwa una maumivu ya kukua wakati unakua. Unajua ninachomaanisha. Ina maana unazidi kuwa mkubwa, kidogo. Unajua, ukichukua, mikono yako itauma. Na miguu yako itauma, unapokua, watoto. Nilikuwa nao. Nilikuwa ninazidi kuwa mkubwa kila wakati. Loo, jamani!

173 Wakati mwingine tunakuwa na maumivu tunapofikia kuwa wanaume na wanawake, tunapozaliwa katika Ufalme wa Mungu, Kristo. Lakini, jambo kuhusu *hilo*, linaumiza; jambo kuhusu *Hili*, linakufanya tu uwe mwenye shangwe na furaha. Ni maumivu ya kukua. Unatoka, unakuwa mkubwa zaidi, unapata kuwa mtu mkubwa zaidi sasa, jinsi ulivyokuwa. Unaweza kuangalia juu ya mambo.

174 Sio tu kuwa na mabega mapana zaidi; hiyo haimaanishi chochote juu yake. Lakini wewe ni mpana zaidi *hapa* ndani, unaona, si *hapa*. *Hapa* ndani, hapa ndipo unapopaswa kupanuka, kuwa mkubwa zaidi, moyoni mwako, upande wa ndani. Kristo anapoingia moyoni, ndipo anaingia kinywani, ndipo anaingia machoni. Anaingia akilini.

175 Anakuja kinywani. Anakufanya uongee tofauti. Huzungumzi kama ulivyozoea kuzungumza. Kristo aliingia kinywani mwako. Imekua sasa kutoka moyoni mwako, upendo wako uliokuwa nao Kwake, hata unaweza kuudhibiti ulimi wako. Ndugu, hilo ni jambo kuu.

176 Kisha, jambo linalofuata unajua, inakua ndani ya macho yako. Jambo linalofuata unajua, unaona, yale mambo ya kale ya ashiki uliyokuwa ukiangalia, utageuza kichwa chako. Unakua.

177 Kisha, jambo la kwanza unajua, bado unageuza kichwa chako, lakini unawaza. Unaona? Baada ya kitambo, inakua katika akili yako; hata hufikirii juu yake tena. Basi wewe ni mvulana mkubwa tu basi. Unakuwa mtu mzima, aliyekomaa, anayeishi kwa ajili ya Bwana. Kwa hiyo, basi, wewe uko ndani ya Kristo basi, kiumbe kipya.

178 Sasa, wakati mitume hawa walipoanza kulipokea Hilo, loo, walikuwa na furaha sana! Wakawazia, "Loo, jamani, hii si ni ajabu!" Na Roho Mtakatifu alikuwa amewajaza, nao walikuwa huko nje, wakiwaponya wagonjwa na kufanya maajabu.

179 Na palikuwa na jamaa mdogo, jina lake Petro, na Yohana. Walipitia langoni, na lilikuwa Zuri, katika mlango wa 3 pale. Na wao . . .

180 Tungekuwa na muda zaidi wa kushughulikia hilo; lakini hatuna. Hatuna budi kufanya haraka sasa, kushuka chini kwa vifungu vichache. Ninaanza historia na kamwe sifikii mlango ambao nilikuwa nikizungumzia. Kwa hiyo, basi, unaingia katika kuifanya. Ni nzuri kabisa! Ni, kila chembe, nzuri. Na ni, kila mahali tu unapoipata, hutaki tu kuiacha. Ni ninii tu . . .

181 Sikiliza, nimesoma Biblia kwa miaka ishirini na mitatu. Na kama sijasoma ila mstari mmoja, ningali ningeweza kuwa nikihubiri kwenye mstari huo mmoja, na somo jipya kila usiku, jambo jipya kila usiku. Unaona, ni halisi kabisa! Imevuviwa. Ikiwa imevuviwa, hakuna . . . Haina mwisho. Ni ya milele, hata milele. Ikiwa Neno moja, "Mimi ndimi Bwana," unaweza kuhubiri juu ya hilo kwa miaka milioni mia moja, na ingekuwa safi tu kama siku iliyosemwa. Unaona, haina mwisho. Inaendelea tu, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea. Hakuna mwisho Kwake; unazidi tu kuendelea.

182 Sasa sikiliza hili. Sasa, wanafunzi, walikuwa na wakati mzuri ajabu. Ndipo Petro akatoka nje mpaka lango liitwalo Zuri, yeye na Yohana. Walikuwa wamepanda kule wakiomba, wakiwa na wakati mzuri sana. Na hapa alilala mtu na kidogo . . . alikuwa kilema. Unajua kilema ni mtu wa aina gani, kidogo—kidogo anatembea kwa shida. Labda alikuwa na yabisi kavu, au kitu fulani. "Alikuwa kilema tangu tumboni mwa mama yake.

183 Petro akatazama, akipitia pale, akiongea na Yohana. Akasema, "Sasa tunaingia hekaluni, kuabudu." Akisema, "Yohana, sasa si tuna wakati mzuri sana?" Au, kitu kama hicho; utukufu moyoni mwao. Kidogo ilibidi waangalie walichokuwa wanasema, kwa sababu wasikilizaji na watu walio karibu, walikuwa wakite- . . . Waliteswa sana.

184 Hapo palikuwa na mtu mmoja, mlemavu tangu tumboni mwa mamaye; maskini, mzee ombaomba. Aliangalia huko nje; na alitaka kitu. Petro alisema, "Sasa, fedha na dhahabu, sina. Sina pesa yoyote. Lakini kile nilicho nacho nitakupa, ikiwa unataka kukikubali." Naye akainua macho akamtazama, kama kupokea kitu. Akasema, "Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama na utembee."

185 Na kwa hivyo mtu huyo asingeweza kutembea. Kwa hiyo Petro akaja tu na kumshika mkono, yeye na Yohana, wote wawili, wakamwinua. Wakasema, "Hukusikia tulichosema? Simama na utembee." Ndiyo hiyo. Huyo mtu akasimama. Na, vema, mbona, akasema . . . Jambo la kwanza unajua . . . Nilimshikilia tu pale kidogo, na mifupa yake ya kifundo cha mguu ikapata nafuu kidogo, naye akaanza kuondoka.

186 Akasema, "Naam, tazama hapa!" Naye huyo akaenda zake. Na muda si muda wajua, akaanza kurukaruka, na kuruka, na kukimbia.

187 Na unajua watu hao walisema nini? Kasema, "Watu hao wana shida gani?" Mbona, waliwaingiza mle ndani na kuwapiga, na kuwaweka gerezani. "Mbona," akasema, "hawapaswi kufanya hivi. Haikuja kupitia kanisani." Haya basi. Sasa mlango wa 4, anza.

> *Walipokuwa wakisema na watu, makuhani,* wakuu *wa hekalu na Masadukayo wakawajia,*

188 Petro na hao wangali wakizungumza na watu. Loo, walikuwa wanazungumza. Sikiliza hapa. Hebu nichukue kifungu kimoja au viwili nyuma ya hii, katika mlango wa 3, kwa namna fulani kuunga mkono jambo hilo kidogo hapa. Hebu tuchukue mstari wa 20. "Naye atamtuma Yesu . . . " Petro akihubiri:

> *. . . atamtuma Yesu . . . ambaye hapo awali mlihubiriwa:*

189 Kupitia manabii na kila kitu, unaona, iliwaambia walipaswa kuipokea, lakini hawakuipokea. Aliwaambia kule nyuma, kasema, "Kwa mikono miovu mmemsulubisha Mkuu wa Uzima." Aliwaambia. Kasema, "Mlifanya hivyo kwa kutokujua, maana Mungu alisema mtafanya jambo hilo."

190 Kwa nini makuhani hao hawangeweza kuamini? Kwa nini watu wa kidini, watakatifu hawangeweza . . . Loo, siwezi kuruhusu hili lipite, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, "Amina. Endelea moja kwa moja."—Mh.] Tazama, watu wa kidini, watakatifu, wakiishi katika kila nuru waliyokuwa nayo, na chochote kile! Watu wa dini, watakatifu, na, "Hawangeweza," Biblia ilisema, "hawangeweza kumwamini Bwana Yesu." Kwa nini? Mungu alilikusudia tangu awali.

191 Isaya akalinena, akasema, "Wana macho . . . " Kasema, "Hawangeweza kumwamini Bwana," kwa sababu Isaya alisema, chini ya uvuvio. Mungu aliishusha kwake, yapata miaka mia nane kabla hawajaja. Kasema, "Wana macho, na hawawezi kuona; masikio, hawawezi kusikia." Na, kwa hiyo, hawangeweza kumpokea Yesu. Haidhuru walitaka kuamini kiasi gani, kulikuwa na jambo fulani ambalo halingewaruhusu, kwa sababu Mungu alikuwa amesema hivyo.

192 Ndugu, unapaswa kuwa ndiye mtu mwenye furaha kuliko wote ulimwenguni, kujua, asubuhi ya leo, kwamba umeketi hapa kama mwaminio wa Bwana Yesu. Ndiyo, bwana, ndugu! Hujui, au mwenye dhambi hajui maana yake, kwamba wakati Mwenyezi Mungu anabisha juu ya moyo wake! Mbona, hakuna kitu kama hicho, popote. Usingeweza . . . Ungeweza kutafuta na kutafuta mbingu, na usingeweza kupata kitu chochote sawa na hicho, kwamba jinsi Mungu mtakatifu, asiye na kikomo

angeshuka na kubisha hodi kwenye moyo wa mlango wa mwenye dhambi, na kutaka kuishi marafiki pamoja naye. Whiu! Inapaswa kutufanya tujiachilie, kila mtu.

193 Sasa ona. Tazama hapa. Alisema, "Ilikuwa kabla ya kuhubiriwa kwenu."

194 Sasa sikilizeni. Hata kabla ya kuzaliwa, au hata kabla ya ulimwengu uliotangulia gharika, ulimwengu uliotangulia gharika, kabla haujaharibiwa kwa maji, Yesu Kristo alihubiriwa kwa watu. Katika bustani ya Edeni, Yesu Kristo alihubiriwa kwa watu. Je, ulijua hilo?

195 Yesu alipokufa msalabani, ili kutimiza. . .Huyo alikuwa ni Yesu, si Roho Mtakatifu ndani Yake. Unaona? Alipokufa msalabani, na nafsi Yake, si Roho wa Mungu, bali nafsi Yake ilienda kuzimu, maana ilimbidi. Biblia ilisema angeenda. Lakini Yesu aliamini kwamba angefufuka katika siku tatu, maana alijua siku tatu uharibifu ungeingia.

196 Naye Daudi akasema, "Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake kuzimu."

197 Yesu alisema, "Uharibuni mwili huu, katika siku tatu utafufuka tena." Ndani ya siku tatu! Hakuwa hapo haswa, hadi dakika, siku tatu. Ilikuwa wakati fulani ndani ya siku hizo tatu, Yeye angefufuka tena. Kwa maana alijua angeenda. . .Mwili wake ungeanza kuoza, maneno ya wazi; ungeanza kuharibika, kwenda mbali, baada ya siku tatu.

198 Naye alijua ya kwamba hakuna chembe hata moja ingeoza, kwa maana alisema, "Sitamruhusu mtakatifu Wangu aone uharibifu." Haleluya! Yesu, kwa Andiko moja, alinena kwa mhubiri aliyerudi nyuma, chini ya uvuvio, aliamini na akaiamini nafsi Yake kwenda kuzimu. Hiyo ni kweli. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

199 Naye akaenda akazihubiri hizo roho zilizokuwa kifungoni, ambao hawakutubu katika saburi ya siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa.

200 Walikuwa na Henoko na wengine wote, na piramidi na kila kitu, walipokuwa wakizijenga. Na kuwahubiria Bwana Yesu Kristo, nao wakakataa kulikubali. Wakiwa wakaidi, wenye kujivuna, na wakakataa kulikubali!

201 Ndipo Yesu akaja kwenye malango ya kuzimu, akasema, "Mimi Ndiye ambaye manabii walisema nitakuwa hapa." [Ndugu Branham anagongagonga kwenye mimbara—Mh.] Haleluya! "Mnaona niko hapa! Neno la Mungu halina makosa. Maelfu ya miaka yamepita, miaka elfu nne, lakini niko hapa. Damu Yangu iko Kalvari asubuhi ya leo. Hakika. Neno la Mungu ni halisi, basi ni kwa nini hamkutubu?" Walipotea na kuhukumiwa.

202 Ndivyo itakavyokuwa wakati Kuja kwa Bwana kutakapokuja tena. Neno la Mungu halikosei. Yale aliyosema yatatukia, hakuna kitu kinachoweza kuyazuia. Hakuna kizuizi kinachoweza kuyazuia. Haijalishi jinsi nyakati zinavyobadilika, jinsi watu wanavyobadilika, jinsi wahubiri wanavyobadilika, jinsi makanisa yanavyobadilika; Neno la Mungu litabaki, litakuja. Atakuwa hapa. Atakuja katika utukufu Wake, pamoja na Malaika Wake wote. Hiyo ni kweli. Neno la Mungu lilisema hivyo.

203 Na siku moja, kila mtu binafsi anayeketi katika chumba hiki, leo, atatoa ushuhuda, akimwona akija katika Utukufu. Atakuja, kwa furaha yako au huzuni yako, moja au nyingine. Hiyo ni kweli. Hana budi kuja. Neno la Mungu halikosei.

204 Kumbukeni ile Sanamu ya Uhuru kule juu, mkononi, usiku ule. Nadhani nimeisimulia hapa hapo kabla. Niliwaona hao shomoro wadogo wamelala pale, karibu na kioo kile kikubwa pale, huku maskini vichwa vidogo vimepigwa vikatoka. Nilimwambia kiongozi, nikasema, "Naam, nini, wao huko?"

205 Alisema, "Naam, walikuwa na dhoruba jana usiku." Naye akasema, "Wakati taa zilipokuwa kwenye Sanamu ya Uhuru, maskini wale ndege wadogo walinaswa kule kwenye dhoruba, na giza. Na badala ya kujaribu kutumia nuru, kuruka hadi mahali salama, waliruka dhidi yake, wakijaribu kuipiga." Sasa, nuru iyo hiyo iliyowafanya wafe, ingeweza kuwafanya waishi, kama wangeitumia ipasavyo. Akasema, "Nao wamelala hapo, kwa sababu akili zao zimepigwa zikatoka. Walikuwa wakijaribu kuiondoa nuru hiyo. Nuru iliyokubaliwa, na kusema, 'asante,' na kuiruhusu iwaongoze; walijaribu kuipiga."

Nikasema, "Mungu asifiwe!"

206 Makafiri watainuka, kanuni za imani zitainuka, watu wakisema, "Biblia si kwe-. . .kweli. Haijavuviwa." Wanapiga akili zao tu. Wakati, wangeweza kuchukua—wangeweza kuwapeleka kwenye Utukufu. Ni Nuru, taa, kwa njia, na kwa watu. Na mwanamume yeyote ama mwanamke ambaye angekubali Neno la Mungu, na kusema, "Huenda nisilielewe, lakini, Bwana, nitatembea ndani Yake hadi kwenye Nuru."

> Tutatembea Nuruni, ile Nuru nzuri,
> Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema
> yanang'aa;
> Tuangazie kote mchana na usiku,
> Yesu, Nuru ya ulimwengu.

207 Hakika, tutatembea katika Nuru. Si kujaribu kulishinda, si kujaribu kusema, "*Hii* si sawa. *Hii* si sahihi. Na, *Hiyo*, hiyo si sawa. Na *Hiyo* si sawa."

208 Ee Mungu, usiniache niipige vita Nuru Yako. Hebu niikubali moyoni mwangu, na kusema, "Ni kweli, Bwana. Nami nitatembea katika Nuru."

209 Hao ndege wangeweza kuchukua nuru hiyo, na kuichunguza moja kwa moja, ilipokuwa ikishuka kupitia pale; na kwenda moja kwa moja kwenye shimo zuri chini ya nyumba fulani mahali fulani, katika makazi mahali fulani, na wangelindwa kutokana na dhoruba.

210 Na ya dhoruba hii kuu ya utaratibu, dhoruba kuu ya kutojali, dhoruba kuu ya kumkana Mungu. "Ee Mungu, usiniache nijaribu kuiondoa Nuru. Hebu niitumie kuingia ndani. Ninaiamini, Bwana." Haya basi. Tembea katika Nuru. "Kama ninavyoiona katika Maandiko, hiyo ni Nuru. Ni Neno la Mungu, basi niruhusu nitembee ndani Yake. Bwana, Bwana, nijalie nienende ndani Yake; kamwe, kamwe nisijaribu kulikana."

> *Naye atamtuma Yesu. . .ambaye mlihubiriwa* hapo awali:
>
> *Ambaye* mbingu *lazima zimpokee, hata* wakati *wa* kufanywa upya *vitu vyote, ambayo Mungu amesema kwa vinywa vya manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.*

211 Kifungu cha 21 cha mlango wa 3, "Kufanywa upya kwa vitu vyote," kutakapokuwa na mbingu mpya, dunia mpya, serikali mpya, uchumi mpya, loo, jamani, mfalme mpya, maisha mapya, mwanzo mpya usio na mwisho, loo, jamani, enzi mpya, wakati mpya, watu wapya.

212 Loo, nina furaha sana nina ahadi ya Mungu, asiyekosea kabisa, hata alikwenda kuzimu kuishuhudia. Mungu yeye yule aliniahidi ningekuwa pale na Uzima wa milele, kwa sababu nilimkubali Mwanawe, Kristo Yesu, na kuamini kila neno alilosema kuwa ni Kweli. Ni lazima tu kuwa huko! Loo, jamani! Ni jambo la ajabu jinsi gani!

213 Jinsi tunavyopaswa kuwa katika upendo pamoja Naye, yule Mtakatifu wa Mungu anayependeza, asiyekosea! Jinsi tunavyopaswa kumpenda, na kuacha kila kitu kingine kiwe cha pili! Kila kitu, hata nyumba yako, hata familia yako, hata kila kitu, hata watu wako wote, kila kitu kingine, ni cha pili. "Yule ambaye hatamwacha baba, mama, dada, kaka, mume, mke, watoto, wala nyumba, chochote kile, na kunifuata Mimi, hastahili kuitwa Wangu. Na ambaye ataweka mkono wake kwenye jembe na hata kugeuka kutazama nyuma, hastahili kulima."

214 Nipe Mafuta katika taa yangu, Bwana. Ee Mungu, nijaze tu tena na tena. Nipatie chanjo kutoka kwa mambo ya ulimwengu. Naomba niwe na kinga dhidi ya mambo yote yasiyo ya kitauwa, ndicho ninachotaka. Jalia Roho Wako Mtakatifu aje kwangu, na anifanye niwe na kinga dhidi ya mambo yote ya ulimwengu.

215 Nataka kumwona Yesu. Nataka kumwona Yesu. Na wewe je? Hiyo ni kweli. Yesu, Mwokozi wangu, kweli kabisa! Lakini nitakapoifikia pwani hiyo kwenye Nchi ya mbali, nikifika

kule katika Nchi mpya, nisijue mtu yeyote, basi nataka kumwona Yesu. Najua nitakuwa na Rafiki Huko. Nawe je? Ndipo Yesu atanionyesha mama, atanionyesha wapendwa wangu, na wapendwa wangu wote karibu nami wakati huo. Hum!

216 Hapo ndipo "kufanywa upya kwa vitu vyote." Unaona? Sikiliza. Hebu nisome hicho tena, kifungu cha 21.

> *Ambaye* mbingu *zinapaswa kumpokea* (hiyo ni, mbingu lazima zimpokee Yesu, unaona) *mpaka* wakati *wa* kufanywa upya *vitu vyote—vitu vyote ambavyo Mungu amesema kwa kinywa cha*. . .*manabii wake watakatifu tangu mwanzo wa ulimwengu.*

217 Loo, jamani! Ni mtu aliyevuviwa jinsi gani aliyekuwa amesimama pale! Hata hivyo, Biblia ilisema, "Alikuwa asiye na elimu wala maarifa." Alimponya mtu kwenye lango liitwalo Zuri, kupitia imani yake katika Jina la Yesu Kristo. Kweli.

218 Nao, hao walimu wa kidini, Madaktari wa Uungu, wenye vyeo vya juu, na mkuu wa kanisa na kila kitu, akasema, "Mfunge mtu huyo! Mtieni gerezani! Kumbe, uzushi huo, ni upuuzi!"

219 Lakini alijua alichokuwa anazungumzia. Walichukua maarifa kwao, wakijua kwamba walikuwa pamoja na Yesu.

220 Ee Mungu, naam, hiyo—hiyo ndiyo elimu ninayoitaka. Kama naweza kuishi karibu vya kutosha na Mungu mpaka wengine waweze kumwona Kristo ndani yangu, na Kristo ndani yako, hiyo ndiyo elimu yote ninayojali. Hapo ndipo ninapotaka kuwa.

221 Sitaki waseme, "Vema, sasa sarufi yake ni nzuri sana, na ana elimu kama hiyo, na anajua theolojia." Loo, jamani! Mungu, ondoa hilo. Si—sininii. . . Sijaipata, na ninaifurahia. Unaona?

222 Acha niwe na Yesu, kufikia mahali nitakapoweza kutembea, na watu wanasema, "Huyo jamaa, simwamini, mimi. . .lakini yeye—yeye hakika amekuwa na Yesu." Hilo, hilo si ndilo unalotaka waseme juu yako? "Mwanamke huyo, msichana huyo, mwanamume huyo, mwanamke huyo, amekuwa pamoja na Yesu. Naam, bwana. Naam, angalia maisha yao. Angalia jinsi wanavyoishi, na angalia jinsi wanavyotembea. Angalia jinsi Mungu anavyowabariki na kuwainua. Na wanapokuwa na makosa yao na kadhalika, namna hiyo, yamekwisha tu, namna hiyo, nao wanaendelea moja kwa moja, hivyo." Loo, jamani, hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Nanyi je?

223 Sasa, kwa dakika kumi, hebu tusome hili, sehemu iliyosalia ya mlango huu, au kuanza mlango huu, hasa, cha 4 kifu-. . . Mlango wa 4.

> *Na alipokuwa akisema na watu*, na *makuhani, na* Masadukayo *wa hekalu, na Masadukayo* (hasa) ndani ya. . .*wa Hekaluni, na Masadukayo wakawajia,*

224 Sasa hawa hapa Masadukayo, ambao hawaamini. Picha halisi ya makanisa leo, ambayo hayaamini katika mambo ya

kimbinguni. Hawakuweza kabisa kuyaamini. Sasa kumbukeni, kumbukeni, kuna watu leo ambao hawaamini katika—Roho Mtakatifu kulitawala na kuliongoza Kanisa. Hawaamini miujiza. Hawaamini ishara. Hawaamini mambo yasiyo ya kawaida. Hawawezi kabisa kuamini hayo. Sasa, roho hiyo si chochote kipya. Hii hapa moja kwa moja juu ya Masadukayo. Waliamini jambo lilo hilo. Unaona, roho hazifi. Watu hufa; roho zinaendelea.

225 Mungu alichukua Roho Wake, akamchukua mtu Wake, Eliya, na sehemu maradufu ya Roho Wake ikaja juu ya Eliya. Je, hiyo ni kweli? Ndipo yapata miaka mia nane baadaye, akaja juu ya Yohana Mbatizaji. Je, hiyo ni kweli? Na inakuja moja kwa moja hadi siku ya mwisho tena. Ye-. . .

226 Mungu alimchukua Mwanawe, Bwana Yesu. Unaamini hilo? Lakini Roho Wake alirudi. Je, hiyo ni kweli? Ilikuwa juu ya Martin Luther. Ilikuwa juu ya John Wesley. Ilikuwa ikiendelea kote katika wakati. Ilikuwa juu ya Sankey, Moody, Finney, Knox, Calvin, hao wote, unaona. Ikashuka moja kwa moja, na sasa inaendelea moja kwa moja leo. Waangalie watoto wao kule nyuma, wanakana tu kila kitu ambacho hao watu waliamini; lakini sio waanzilishi.

227 Niliposimama si muda mrefu uliopita kando ya yule mwanzilishi mkuu aliyesimama pale, nilitazama na kuwaza, "Ee Mungu, angalia pale, Dwight Moody." Niliwazia, "Tazama hapa juu. Na mtu huyo, mambo aliyoyaamini; nguvu za Mungu, za kimbinguni. Hajasoma! Vitabu vyake unavyosoma, unaona ni nani aliyeviandika. Aliviandika, yeye mwenyewe, lakini ni nani aliyeyapiga msasa? Sarufi yake ilikuwa mbaya sana. Alikuwa na elimu ya daraja la tatu hivi, na maskini fundi wa kushona viatu. Lakini, ndugu, alileta watu nusu milioni kwa Mungu. Unaona? Ilikuwa ni nini? Wangemfukuza kanisani, na kusema yeye alikuwa mlokole na kila kitu kingine. Lakini alitoka na kuona kundi la watu. . .

228 Alikuwa na ujumbe moyoni mwake. Ilibidi ahubiri sana, hakujua la kufanya. Basi akaenda akanunua sanduku la viatu kwa mtu; mbao, maskini sanduku kubwa la kiatu, lililotengenezwa kwa mbao. Akalipa senti kumi kwa ajili yake. Akaliweka kwenye kona. Na wanaume hawa wakipita. Alisimama pale na kuhubiri, moja kwa moja kwenye kona, kwao, namna hiyo. Hiyo ni kweli. Nami nawazia juu ya kanisa alilokuwa nalo, na angalia Biblia ya Moody leo.

229 Ndipo nikawazia, "Mwangalie John Wesley!" Niliposimama mahali pale pale alipofia mtu huyo. Nilikuwa na vazi lake alilokuwa amevaa, limetiwa nta. Waliliweka juu ya mabega yangu, kwa heshima tu ya kuwa pale, nilipomwombea mfalme. Wakati. . .Na kuliweka kwenye mabega yangu. Nilisimama

mimbarani mwake, mahali ambapo angeenda kila asubuhi saa kumi na moja, na kuwahubiria watu elfu moja na mia tano.

230 Niliketi kwenye kiti chake, ambapo alishinda mpiganaji wa kuku ambaye. . .jamaa aliyezoea kupigana, kuwa na vita vya jogoo. Alimleta kwa Kristo. Nacho kilikuwa na ngozi juu yake, hivi, na pembe mbili kubwa, na mahali kama *hapa* palipowekwa upande huu kama *hapa*, ambapo wangeandika rekodi ya mapigano. Na baada ya Wesley kuongoka, Wesley alimleta mtu huyu kwa Kristo, kisha akampa kiti hicho. Nami nikaketi kwenye kiti hicho na—na kuomba.

231 Niliketi kwenye tandiko lake ambapo, alikuwa papa hapa Marekani, alikuwa na chumba chake kidogo cha siri nyuma yake, wakati angeketi kinyumenyume juu ya farasi wake, akageuza milipuko yake namna *hii*. Na akiwa njiani akija hapa, pamoja na Asbury na hao, angeketi pale na kuandika jumbe zake na kadhalika, namna hiyo, kama vile Mungu angempa. Kwa vile hakuweza hata kuchukua muda kusimama popote, alipanda farasi wake, papa hapa Marekani, ameketi kwenye tandiko. Nami niliwazia, "Ee Mungu!"

232 Nilisimama pale ambapo alijengewa kumbukumbu hiyo. Ambapo, wakati mmoja, akihubiri uponyaji wa Kiungu, na kanisa kuu la Uingereza lilimfungulia mbweha, na majibwa makubwa huko juu, na kumpitisha katikati wakati Wesley alipokuwa akihubiri uponyaji wa Kiungu. Na Wesley akanyoosha kidole chake usoni mwake, na kusema, "Jua halitatua, juu ya kichwa chako, mara tatu, nawe utaniita nikuombee." Na mtu huyo akafa jioni hiyo akiwa na mkakamao tumboni, akimwita, Wesley aje amwombee.

233 Mtu huyo huyo; unaweza kuketi katika kanisa lako na kusikia Dr. Church na wao, mafundisho yale yale ya kanisa lile lile lililoamini jambo lile lile, yanakataa Biblia kuwa imevuviwa. Mungu akurehemu. Sitaki shirika lolote.

234 Lakini nisaidie kuishi ili katika kizazi changu. . . Sitasimama katika kizazi kingine. Sitakuwa na chochote cha kuwahukumu. Sitalazimika kusimama hukumuni pamoja nao. Lakini itabidi nisimame kwenye hukumu pamoja na wanaume na wanawake ambao nimeishi nao. Hapo ndipo inapojalisha, kule katika ufufuo, siku zangu zitakapokwisha na nimefanya niwezavyo, kama mimi ni mtumishi wa Mungu. Mungu atamwinua mtu mwingine katika siku hiyo nitakapoondoka. Kwa hiyo hakuna haja ya mimi kuweka kitu karibu na theolojia yangu; ni mimi kuishi katika Nuru niliyo nayo, na kungoja mpaka. . .juu ya Mungu. Kwa ajili ya kizazi kijacho, Yeye atakuwa na mtu hapo wakati kizazi hicho kitakapotokea. Amina. Loo, jamani!

235 "Kuwa na huzuni." Wasikilize Masadukayo hawa.

*Wakiwa na huzuni kwa kuwa waliwafundisha watu, na kuhubiri kwa njia ya Yesu ufufuo* wa *wafu,* ule usio wa kawaida.

236 "Loo," wanasema, "hiyo ni . . . Loo, tunaamini katika ufufuo wa wafu. Lakini sasa, uponyaji wa Kiungu na mambo mengine, hayo hayako." Mbona, ni ibilisi yule yule. Ni kitu kile kile. Unaona?

237 Sasa, siku hizo, walisema, "Loo, tunajua Yeye anaweza kuponya. Lakini anajifanya Mungu, anaposamehe dhambi." Sasa ibilisi yuyo huyo aligeuza tu, aseme, "Leo anaweza kusamehe dhambi, lakini hawezi kuponya."

238 Ikiwa Yeye ni Mungu, anaweza kuponya, kuokoa, kusamehe dhambi, au chochote. Anabaki kuwa Mungu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Tazama.

*Wakawakamata, wakawaweka gerezani* hata *siku ya pili yake: kwa maana ilikuwa* jioni.

*Lakini wengi katika wale waliosikia lile neno waliamini; . . .*

239 Kwa nini? Kwa nini baadhi yao waliamini, na wengine hawakuamini? Loo, ndugu, wengine walikusudiwa Uzima wa milele, na wengine walikusudiwa hukumu ya milele. Hiyo ndiyo sababu. Hiyo ndiyo hasa. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja, isipokuwa Baba Yangu amwonyeshe kwanza. Baba Yangu . . . "

240 Samaki angewezaje kuuma kwenye chambo cha kasa? Unaona? Hawezi. Hamu ya samaki ni tofauti na hamu ya buibui wa majini. Nyoka na samaki hawana chakula sawa. Unaona ninachomaanisha? Naam, bwana. Samaki daima ni kitu kimoja, kwa maana alizaliwa samaki. Daima atakuwa samaki. Na mtu huyu anaweza kufasiri . . . Huenda kasa huyu akataka kuwa samaki. Kasa ana nyama ya samaki ndani yake, lakini yeye si samaki. Ana nyama nyingine ndani yake, pia. Yeye hatawahi kuwa samaki. Hapana, bwana. Wala samaki hatakuwa kasa. Kwa maana alianza, kasa, atabaki kuwa kasa. Naye alianza, samaki, atabaki kuwa samaki.

241 Na kila mwanamume ama mwanamke, haleluya, ambaye amewahi kuzaliwa kabisa na Roho wa Mungu, unaweza kurudi nyuma. Naam, bwana. Unaporudi nyuma na kuenda nje, utakuwa mtu mwenye mashaka zaidi ambaye umewahi kuota maishani mwako, mpaka urudi. Na ukikosa kufanya hivyo, Mungu ataondoa uhai wako duniani. Mungu aliahidi kufanya jambo hilo.

242 Hapa si muda mrefu uliopita, niliingia kwenye Gereji ya Vorgang hapa chini, nami nilikuwa nikizungumza na mhubiri mzuri ambaye ni jirani yangu hapa. Na siku zote nimekuwa na heshima kubwa kwa mwanaume huyo. Alikuwa mtu mwema,

mhubiri mzuri. Alitembea kwenye mitaa hii wakati wa kudorora kwa uchumi, akiuza bidhaa za Rawleigh, apate kuhubiri Injili. Naam, bwana.

243 Mtu fulani alimdhihaki, papa hapa kwenye Barabara ya Saba, kasema, "Kwa nini usifanye—usifanye *hivi-na-hivi*?"

244 Akasema, "Mheshimiwa, haya ni maisha halali." Akasema, "Ninauza hapa, bidhaa fulani, na vitu kama unga wa keki, chochote kile, kufanya niwezavyo, kwa maana mimi ni mhudumu wa Injili." Papa hapa katika church of God; ilikuwa ni Ndugu Ramsey. Naye akasema, "Ninafanya vizuri niwezavyo." Na hivyo akamwambia mtu huyo. Kwa kweli alizaliwa kwa Roho wa Mungu.

245 Niliingia kwenye Gereji ya Osborne hapa chini, siku moja. Akasema. . . Nikasema, "Mungu akubariki, Ndugu Ramsey." Nikasema. . . Alikuwa mtu maskini. Nikasema, "Angalia gari langu kuukuu hapa; inabidi niende safari." Nikasema, "Nilikuwa tu na wakati mzuri." Nikasema, "Laiti ungekuwa pamoja nami, Ndugu Ramsey."

Akasema, "Vema, nadhani, ingekuwa sawa, Billy."

246 Nikamtazama. Nikawazia, "Hiyo haisikiki sawa." Unajua, unaweza kujua wakati kitu kinatokea. Nikamtazama.

247 Akasema, "Ndugu Branham, nadhani unajua simtumikii Bwana tena."

Nami nikasema, "Ati nini?" Ni—nikasema, "Sasa unanitania."

Akasema, "La, simtumikii Yeye tena."

248 Naam, nilifikiri bado ananitania tu. Nikatoka tu. Nilienda nyumbani. Nikamwambia Meda kuhusu hilo. Nikasema, "Ndugu Ramsey aliniambia hamtumikii Bwana tena. Kuna kitu kuhusu hilo, Meda, ambacho si sahihi kabisa."

249 Ilinisumbua. Nikarudi chini tena. Nikasema, "Ndugu Ramsey, njoo hapa, nataka kuzungumza nawe kwa dakika moja."

Akasema, "Sawa, Billy."

250 Nikaenda huko. Nikasema, "Ndugu Ramsey, nilikuwa hapa ndani siku chache zilizopita, nawe uliniambia kuwa humtumikii Bwana tena." Nikasema, "Ulikuwa unanichezea, sivyo?"

Akasema, "Hapana, hapana."

251 Nikasema, "Ndugu Ramsey, unamaanisha humtumikii Bwana tena?"

Akasema, "Hapana." Akasema, "Nilirudi nyuma."

252 Nikasema, "Vema, Ndugu Ramsey, afadhali umrudie Mungu." Nikasema, "Njoo, uende pamoja nami mkutanoni."

253 Akasema, “Hapana, Billy.” Kasema, “Si—sijali kabisa kumtumikia Yeye tena.” Akasema, “Ninaninii tu . . . ”

Nikasema, “Unamwamini?”

254 Akasema, “Loo, ninamwamini, lakini simtumikii tu. Niliacha.” Akasema, “Kumekuwa na mambo mengi sana.”

Nikasema, “Ndugu Ramsey, usiangalie mambo. Mwangalie Yeye.”

255 Naye akasema, “Vema, Ndugu Branham,” akasema, “Mimi simtumikii tu Bwana, na ni afadhali nisiongee juu yake.”

Nikasema, “Vema, ndugu, Mungu awe pamoja nawe, akusaidie.”

Ndipo siku chache baada ya hayo, akawa mgonjwa.

256 Mhudumu mwingine, sitataja jina lake, maana sina hakika. Ninaamini ameketi nyuma sasa hivi. Mhudumu huyu alimwendea, rafiki. Akasema, “Ndugu Ramsey, hutaki kuja, kumtumikia Bwana?”

257 Akasema, “Hapana.” Mungu akimpa, kupitia kwa wajumbe Wake, nyakati zote mbili, maonyo. Alisema, “Hapana.” Baada ya saa chache kutoka hapo, alimchukua mikononi mwake, na akaenda Nyumbani. Mungu alimwondoa duniani. Naam, bwana.

258 Unakumbuka, Paulo, yale aliyowaambia kule, mtu huyu ambaye hangeitii Injili? Alisema, “Mkabidhi kwa ibilisi, kwa uharibifu wa mwili wake, ili nafsi yake iokolewe.” Hiyo ni kweli. Huwezi kucheza na Mungu. Ndugu, Neno hilo limevuviwa, kila Neno Lake, liko moja kwa moja kwenye mstari wa kuchongea. Hiyo ni kweli. Ama utafuata mkondo . . . Lakini kama umewahi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, wewe ni mwana wa Mungu.

259 Sasa, ingia. Hua na kunguru, wote wawili, walikuwa ndani ya safina. Hiyo ni kweli.

260 Walipomfungua maskini kunguru; hebu tufananishe hiyo kama kurudi nyuma. Maskini kunguru akaruka kutoka kwenye mzoga mmoja hadi mwingine, na kudonoa kwenye mizoga ya zamani iliyokufa. Alikuwa sawa. Haikuleta tofauti yoyote kwake, maana alikuwa kunguru, kwanza kabisa. Asili yake, hamu yake ya kula, matumbo yake yangeweza kumeng’enya kitu kama hicho. Kwa nini? Alizaliwa na matumbo ya aina hiyo. Unaona, nyongo yake na kadhalika vingefanya maskini mizoga hiyo . . . na kumfanyia chakula. Lakini wakati . . . Aliridhika.

261 Na vivyo hivyo na kila mtu, sijali ni muda gani umekuwa kanisani, na kukufungulia ulimwengu; kama bado unaweza kutoka na kufanya mambo uliyowahi kufanya, na kufurahia, inaonyesha hujawahi kumjia Mungu.

262 Lakini alipomfungua hua, kuona angefanya nini. Hua hana nyongo yoyote. Hawezi kumeng’enya vitu hivyo. Na kama angevila, vingewaua. Lakini hua, angejaribu kuruka

chini; "whiu" asingeweza kustahimili. Angejaribu kuruka chini; "whiu" hangeweza kustahimili. Alitua kwenye kichaka kidogo, apate kupumzika. Naye alikuwa na jani la mzeituni mkononi mwake; alirudi na kugonga mlango. "Baba Nuhu, fungua niingie. Siwezi kuvumilia hapa nje."

263 Kila mwanamume ama mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, hakika, unaweza kurudi nyuma. Lakini, ndugu, kama wewe ni mtoto wa Mungu, huwezi kustahimili mambo ya ulimwengu tena, kwa sababu mambo yako ya kumeng'enya yamebadilishwa.

Petro alisema, "Bwana, twende wapi?"

264 Aliposema, "Je, mnataka kwenda pia?" Wakati wengine wao waliondoka.

265 Akasema, "Twende wapi? Tufanye nini? Wewe pekee Ndiye uliye na Uzima wa Milele. Basi twende wapi?"

266 Huyu hapa, amesimama hapa katika nguvu Zake, ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu, mtume na nabii sasa. Haleluya! Loo, jinsi ninavyopenda kuiona! "Lakini baadhi yao waliamini," kwa sababu walikuwa Nayo, walichagua Uzima wa Milele, wakati mhubiri huyu alipohubiri.

267 Alifanya nini, Ndugu Neville? Moja kwa moja miongoni mwa kundi hilo la wanafiki wanaopiga mayowe, moja kwa moja miongoni mwa kundi hilo la mbwa-mwitu ambao wangemvuta, kipande kwa kipande, kwa sababu ya mapokeo ya kidini! Petro alitupa wavu wake, hapa ndani, akasema, "Huenda kuna samaki huko." Hiyo ni kweli. Alipotupa wavu wake pale, akaanza kuuvuta. Akasema, "Mungu wa baba zetu, aliyekwenda pamoja na Ibrahimu kutoka Uru, akaingia Ukaldayo," ndio, bwana, "amemtuma Mwanawe, Bwana Yesu, ambaye Mbingu lazima zimpokee mpaka kurejeshwa kwa vitu vyote." Akasema jinsi wao. . . Akasema, "Mlimchukua Mfalme wa Amani, kwa mikono ya kikatili, na kumwua na kumsulubisha." Akasema, "Kwa imani katika Jina Lake, mtu huyu ameponywa." Hiyo ndiyo sababu ninaamini katika mambo yasiyo ya kawaida.

268 Akatupa wavu wake pale, naye akauvuta. Naye alipofanya hivyo, hata hivyo baadhi yao mle ndani walikuwa ni samaki. Wengine, kasa, waliendelea pamoja na nyoka na kadhalika. Waliruka wakarudi. Lakini kulikuwa na samaki mle, pia. "Hata hivyo wengi waliamini Neno." Walikusudiwa Uzima wa Milele. Naam, bwana. Waliamini!

*. . . na idadi ya . . . wanaume ilikuwa kama elfu tano.*

269 Jinsi alivyopata wavu uliojaa! Ndiyo, bwana. Labda kati ya milioni, lakini alipata—alipata elfu tano kutoka kwake. Angalia, hajali ilikuwa ni bwawa la aina gani. Alitupa wavu wake moja kwa moja ndani yake. Hiyo ni kweli.

270 Nasi hatujali kama ni wauzaji pombe haramu, kama ni makahaba, chochote kile. Tupa wavu! Hujui ni wa nani aliye chini humo. Hujui. Huwezi kujua. Hakuna mwanadamu anayeweza kujua. Lakini unaweza kutupa wavu, na kuwavuta hadi madhabahuni, useme, "Hii hapa, Bwana. Nimefanya sehemu yangu sasa." Ikiwa ni . . . Na kama yeye ni samaki, tangu mwanzo, atakuwa samaki milele. Naam, bwana. Ikiwa ni buibui, tangu mwanzo, atakuwa buibui milele. Ikiwa kuza- . . . Mwana aliyezaliwa upya wa Mungu aliye hai anashusha Nguvu Zake chini na kumkamata mtu huyo madhabahuni, wavu wa Injili uko karibu. Tazama.

> *Ikawa* asubuhi, *kwamba wakuu, na wazee, na waandishi,*
>
> *Na* Anania, *kuhani mkuu, na Kayafa, na Yohana, na Aleksanda, na . . . watu wengi wa jamaa ya kuhani mkuu walikusanyika huko Yerusalemu.*
>
> *Wakawaweka katikati, wakawauliza, Ni kwa nguvu gani na kwa jina gani mmefanya haya?*

271 "Je, wewe ni Mbaptisti? Je, wewe ni Mpresbiteri? Unaona? Kwa nguvu gani? Wewe ni wa kanisa gani? Mamlaka yako ni nini? Ulitoka seminari gani? Wewe ni nani, hata hivyo? Nionyeshe stakabadhi zako. Hebu tuone wewe ni nani." Kitu kile kile. "Ni kwa mamlaka gani mmewaweka wanaume hapa nje wanaohubiri namna hiyo? Je, uko hapa kwa jina la Sanhedrin? Uko hapa kwa jina la—la Masadukayo, au Mafarisayo, au Maherodi, au watoza ushuru? Au, wewe ni nani?" Haya basi. " . . . umefanya hivi?"

272 "Na, Petro, akiwa mbichi tu kutoka kwenye seminari"? Kifungu cha 8. "Petro, na Shahada yake ya kwanza, na shahada yake ya Udaktari"? La. Loo, jamani! Biblia haisomi hivyo. Hiki ndicho kilichompata Petro:

> . . . *Petro, akiwa amejazwa na Roho Mtakatifu,* . . .

273 Loo, alikuwa amekua. Si mahali padogo tu namna *hiyo*; alikuwa amekua kabisa. Amejazwa! Kitu chochote kilichojazwa kimejaa kabisa. Petro, hakunyunyiziwa Roho Mtakatifu, bali, "Petro, akiwa amejazwa na Roho Mtakatifu."

274 Sasa hebu tuone utawaambia nini. Sasa kuwa mwangalifu unachosema, maana wanaweza kukufunga gerezani, kijana. Wewe ni—wewe ni mwendawazimu wa kidini sasa, wanavyofikiri. Sasa, wacha tuone, unafanya watu wabadili imani, unafanya kila kitu, kwa hiyo kuwa mwangalifu sana unachosema.

> Lakini *Petro, akiwa amejazwa na Roho Mtakatifu, akawaambia, Enyi watawala wa watu, na wazee wa Israeli,*

*Kama tukiulizwa leo habari ya jambo jema alilofanyiwa yule mtu dhaifu, jinsi alivyoponywa;*

*Na ijulikane kwenu nyote, na kwa . . .watu wa Israeli, kwamba kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye* ninyi *mlimsulubisha, ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, kwa huyo mtu huyu anasimama hapa mbele yenu akiwa mzima.*

275 Whiu! Unaweza kuwazia mtu akijaribu kuweka aina fulani ya the—theolojia ya kamusi juu ya mtu kama huyo? Ndugu, alisimama, ametiwa mafuta na kujazwa na Roho Mtakatifu. Akasema, "Mbona, ninyi watawala, nguvu yenyewe ya Mungu ambayo mnakiri kuwa, Mungu yuyo huyo alimfufua Mwanawe Kristo Yesu, ili kuonyesha mambo yasiyo ya kawaida. Na ninyi, kwa mikono ya uovu, mmemsulubisha."

276 Huna haja ya kumpigilia misumari msalabani. Mkane tu, unamsulubisha tena. Wanafanya jambo lilo hilo leo hii. Mnamsulubisha!

277 Kasema, "Ijulikane kwenu." Kwa maneno mengine, "Mungu yule yule ambaye umedai kuwa unamwakilisha, amemwinua mvulana huyu." Hao hapo. Kasema, "Ni kwa Yeye mtu huyu anaishi. Tukichunguzwa kwa yale tuliyomtendea mtu huyo," kasema, "ijulikane kwenu, si sisi. Lakini ni kupitia kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ambapo mtu huyu anasimama mzima, leo."

278 Sasa hebu niwaambie ni nini kingine alichosema hapa. "Hili ndilo Jiwe . . . " Loo, loo, ndugu, je, ataisugua iingie sasa!

*Huyu ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, ambalo limekuwa jiwe kuu la pembeni.* (Sikiliza.)

*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote: kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu liwapasalo kuokolewa kwalo.*

279 Ndugu, napenda tu Petro akihubiri papo hapo. Aliwaambia nini, kwa maneno mengi sana? "Je, hamjui nabii Isaya, na wengine wengi, walisema kwamba wajenzi watalikataa Jiwe la Pembeni?" Kwa maneno mengine, "Hili ndilo jambo lile lile, wewe kukataa ni jambo lile lile ambalo Mungu alisema ungefanya. Je, hujui wewe ni sehemu yake?"

280 Na hebu niseme kwa kicho, na niseme kwa heshima, hebu niseme kwa upendo wa kiungu, siku ii hii, ndugu na dada yangu wapendwa. Jambo lile lile ambalo Biblia ilisema ya kwamba watu hawa wangefanya katika siku za mwisho, "Kuwa na mfano wa utauwa, lakini wangekana Nguvu zake," hao hapo. Jiwe la Pembeni, limekataliwa. Loo, jamani! Hakika, ninaamini katika mambo ya kimbinguni.

Alisema, "Wala hakuna wokovu chini ya jina lingine lolote."

281 Naomba, badala yake, asubuhi ya leo, nisimame na kunukulia kizazi hiki, "Kwa maana mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuelewa mambo haya, Ufalme wa Mungu," kama alivyomwambia Nikodemo wa kale.

282 Huwezi kuuelewa, hutauelewa kamwe, mpaka Mungu atakapokuja moyoni mwako. Nawe utakuwa sehemu Yake, kisha utasema, "Naam, Bwana, kila sehemu ya Neno imevuviwa. Ninaamini kila sehemu Yake. Ninaamini ni Kweli. Nami hapa, Bwana, kutembea katika Nuru." Mradi tu wewe ni mkwamia mpakani huko nje, huwezi kuamini Hilo. Huwezi. Bwana na akusaidie, asubuhi ya leo, kuona mambo ya kimbinguni.

283 Na utambue jambo hili, kwamba Waebrania 13:8, ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele." Kumbuka, ahadi Zake ni nzuri tu leo kama zilivyokuwa wakati huo; kila kanuni, kila Neno la Mungu ni la lazima vile vile.

284 Na sijali, ndugu, ni watu wangapi wanaolikosoa, ni wangapi wanasema sivyo.

285 Ningeweza, leo, kwa rehema za Mungu, kuleta watu elfu kumi, wakisimama hapa, ambaye wakati fulani alikuwa akifa kwa kansa, ambaye wakati fulani alikuwa kipofu, ambaye wakati fulani alikuwa kilema, ambaye wakati fulani alikuwa hivi; katika miaka michache iliyopita ameponywa, kwa Nguvu za Mungu aliye hai. Na hili ndilo jambo lile lile ambalo Yesu Kristo alisema lingetukia katika siku za mwisho.

286 Na hakika kama Yesu alivyosema uponyaji huu ungetukia, alisema kutakuwa na wakosoaji kwa nje, wanaoidhihaki, na chochote kile. Wote wawili, walikusudiwa Uzima wa milele, nami ni . . . kwa Uzima wa milele au hukumu ya milele.

287 Nina furaha sana, leo, kujua ya kwamba Mungu yuko katikati yetu, na sauti ya Mfalme iko hapa, sifa za Mungu.

288 Kuna mara nyingi nimeshindwa kuomba maombi ya imani. Kuna mara nyingi nimejaribu sana, na kushindwa kulifanya, kwa sababu imani yangu haingeweza kulifikia. Hilo halibadilishi Neno la Mungu hata kidogo. Kama nikiwaombea watu elfu kumi leo, na elfu kumi wafe asubuhi, kesho usiku ningekuwa hapa nikiombea wagonjwa, vile vile tu, kwa sababu Neno la Mungu lilisema hivyo. Hiyo ni kweli.

Ninaamini katika dini ya zamani,
Ninaamini katika furaha ninayoijua;
Ninaamini kuwa njia tunayotembelea,
Ni njia ambayo baba zetu walipita.

Loo, nipe dini hii ya zamani,
Loo, nipe furaha niwezayo kujua;
Kwa maana ninaamini katika dini ya moyoni,
Kama baba zetu walivyopokea zamani.

289 Amina. Ndugu, acha nife nikiwa kazini. Acha niende kama mtumishi wa Mungu. Niishi au nife, ninaamini Neno la Mungu lisiloweza kukosea ni Kweli. Nalo linafundisha uponyaji wa Kiungu, na ishara, na maajabu, na miujiza, kuonekana katika siku hizi za mwisho. Na ninaweza kulithibitisha kwa Neno la Mungu, na ninaweza kuuonyesha ulimwengu, ambapo limetenda kazi. Na kama litaanza kufanya kazi huko nje, kwa nini lisianze kufanya kazi kwako? Yesu alisema, "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana."

Na tuombe.

290 Baba Mungu, tunakuja kwako katika nuru ya Neno Lako, na katika Uweza wa Roho Mtakatifu, ambao umetujalia, Bwana, umetujalia kutoka Juu, kuwa watumishi Wako. Na tunakupenda Wewe. Nasi tunajua kwamba Wewe unatupenda, kwa sababu umetuchagua. Ulisema, kupitia Mwanao, Yesu, "Hamkunichagua Mimi, bali niliwachagua ninyi. Mtu haji kwa Mungu, ila kwa njia ya Kristo. Na hakuna mtu awezaye kuja kwa Kristo, isipokuwa Mungu amvute kwanza."

291 Kwa hiyo, Baba, tunakupa Wewe sifa. Kwako naunyenyekeza moyo wangu, Bwana. Ee Kristo wa Mungu, ondoa yote, kutoka moyoni mwangu, ambayo si vile ungetaka uwe, Bwana. Na iwe kwa ajili Yako tu, na kwa utukufu Wako. Nakupenda Wewe, Bwana wangu.

292 Nami ninaomba ya kwamba utawabariki hawa, watu Wako hapa asubuhi ya leo, kila mmoja wao. Wengi wao hapa ambao ni wagonjwa, Bwana. Wanao watu wagonjwa. Wanauliza maombi. Na, Baba, loo, kwa miaka hii, tangu nimekujua Wewe, nilikuamini Wewe kama mponyaji mkuu. Umelithibitisha hilo, kuzunguka na kuzunguka ulimwengu, Bwana, ya kwamba Wewe ndiwe Bwana Yesu uliyefufuka kutoka kwa wafu. Sasa ninaomba, Baba, ya kwamba utawabariki watu hawa hapa asubuhi ya leo. Bariki.

293 Ikiwa kuna mtu ambaye hajaokolewa hapa, naomba wamwamini Bwana Yesu Kristo sasa. Haidhuru kama ningemleta hapa madhabahuni, kama hawajakusudiwa Uzima wa Milele, ingetupa tu wavu, ni hivyo tu. Lakini, Baba, kama vile Petro alivyolihubiri Neno, na kusema, "Wote walioamini, waliongezwa kwa Kanisa." Baba, ninaomba kwamba leo uongeze idadi katika Kanisa Lako. Tujalie. Jalia watu wengi waamini Hili na kuona ya kwamba ni Kweli. Wako hapa asubuhi ya leo kwa kusudi fulani. Nami naomba ya kwamba umewakusudia Uzima wa milele. Na jalia waupokee leo, kupitia kwa Yesu.

294 Nami ninawaombea wagonjwa, ninapowaleta kwenye madhabahu sasa, kuwaombea, kuwapaka mafuta, mimi na mzee Wako. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utatupatia neema

machoni Pako. Jalia, kwa upande wetu, kwamba kutakuwa na imani isiyoweza kushindwa.

295 Neno la Mungu, ambaye, hata baada ya maelfu ya miaka, na wale ambao wamekufa kwa miaka elfu nne, Yesu alienda kuwaambia kwamba Neno la Mungu limethibitishwa duniani. Jinsi lisivyoweza kukosea!

296 Nawe umesema, "Waweke mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Agizo la mwisho, maneno ya mwisho yaliyotoka katika midomo Yako mitakatifu, Neno la Mungu lililovuviwa. Ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wataweka mikono juu ya wagonjwa; utapona."

297 Na, Baba, wanapowaleta wagonjwa hapa, wenyewe, asubuhi ya leo, kuombewa. Naomba, tukiwawekea mikono, tukiwapaka mafuta, kulingana na Neno Lako, ya kwamba kila mmoja wao ataponywa. Jalia kwamba imani yetu iwe sahihi, na imani yao iwe sahihi. Imetiwa nanga hasa kwenye Neno ambalo limehubiriwa asubuhi ya leo, Neno la Mungu aliye hai. Na ujitwalie Mwenyewe utukufu. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Inakuja ambapo umande wa rehema unang'aa;
Tuangazie kote mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri,
Huja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'aa;
Tuangazie kote mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

298 Samahani nimewacheleweshа. Sasa watoto wadogo wana zawadi ya shule ya Jumapili hapa, katika dakika moja tu. Wana, loo, masanduku ya peremende, na machungwa, na gunia la vitu hapa kwa ajili ya watoto wadogo, mara tu tunapomaliza sehemu takatifu ya ibada, kwa dakika moja tu.

299 [Dada mmoja katika kusanyiko anasema, "Ndugu Branham?"—Mh.] Naam. Naam. [Sehemu tupu kwenye kanda.]

300 Kuna kitu, nami ninaamini ni mtoto huyu. Kwa hiyo, basi, ukiinamisha kichwa chako.

301 Mungu Mwenyezi, sijui. Wewe wajua kwamba yote ni kitu, kwangu, siwezi kuelewa. Sijui. Lakini, Baba, inaonekana, ya kwamba baada ya ujumbe huu, na ujio huu, mtoto huyu akija hapa, na mimi kuangalia katika uso wake; na kulingana na kile nilichoambiwa, mahali fulani, na shahidi wa Dada Cox, na Roho Mtakatifu hapa madhabahuni. Sijui; si zaidi ya nilivyojua siku ile nilipotembea na yule mzee mweusi ambaye alikuwa kipofu. Wala siwezi kuelewa sasa, Bwana; si zaidi ya yule mvulana katika Ufini, aliyefufuliwa kutoka kwa wafu. Wala sielewi kesi

ya hii; na ungewezaje kuiweka juu ya moyo wa daktari, kumtuma hapa. Roho wako akitembea!

302 Sasa, Baba, kwa kutii yale uliyoagiza yafanywe, na kulingana na Neno ambalo nilihubiri kwa bidii sana asubuhi ya leo, kama muumini, ninaenda mbele kumpa changamoto shetani ambaye amemfunga mtoto huyu. Ninaweka mikono yangu juu ya kichwa chake, na juu kwenye macho yake madogo; nikiinua mkono wangu kwa Mungu, ambaye ninamwamini, ambaye amenena na haliwezi kushindwa. Ninaomba kwamba kansa katika macho ya mtoto huyu itoke.

303 Na uende katika giza la nje, ambapo ndipo mahali pako, wewe mwovu wa giza, katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu, ninayemwakilisha.

304 Na macho ya mtoto huyu yawe ya kawaida. Mama arudi, akitoa sifa na utukufu kwa Mungu, kwa uponyaji wa mtoto huyu. Hili ninafanya kwa imani ya kweli kwa Mungu, nikiamini Neno Lake, kulifundisha. Na nikiamini ya kwamba ono limenigusa, mtumishi Wake, nikisimama mahali papa hapa. Na, Bwana, unajua unachoweka moyoni mwangu sasa hivi. Nami naomba Maneno Yako yatimizwe, na maisha ya mtoto huyu yaokolewe, na apate kuishi na kuwa na afya njema na nguvu, na aweze kuona tena, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

305 Dada, mpendwa, bila kujua kile wakati ujao unashikilia, bali nikiamini. . .Hapa, inakuja kwangu. Hii hapa. Ilikuwa iwe ni kitu. . .Papa hapa ndipo jeneza la mke wangu lilipowekwa, Hope. Na ilikuwa asubuhi ya leo. Na ilikuwa ni—ilikuwa ni Hope ndiye aliyefufuka na kusema hatakufa. Na jambo hilo, naamini, lilikuwa na maana kwa mtoto huyu sasa. Amelala mahali pale pale hasa. Na karibu naweza kusema hakika ni BWANA ASEMA HIVI.

306 Mama, sikujui, lakini ninaamini mtoto huyo atafufuka na kuishi, na kuwa mzima. Mungu akubariki. Umeniruhusu nisikie kutoka kwa mtoto wako.

307 Jina lako nani? [Dada huyo anasema “Bibi Bowen,” na anaanza kueleza chanzo cha hali ya mtoto wake. Pia anasema, “Imani yangu inaanza kuyumba kidogo. Na, unaona, nilimkosea, na nikamkosea Mungu, pamoja na hilo.”—Mh.] Ndiyo, ulimkosea Mungu, wewe mwenyewe.

308 [Dada huyo anaendelea kueleza historia ya hali ya mtoto wake. Pia anasema, “Yote yanawezekana, amini tu.”—Mh.] Huo ndio wimbo wangu wa mada, pia, “Yote yanawezekana, amini tu.”

309 [Dada huyo anaendelea kueleza historia ya hali ya mtoto wake. Pia anasema, “Mungu ninayemjua anaweza kuponya.”—Mh.] Naam, dada. Naam. Unaona?

310 Na sasa, unamwahidi Mungu, unaposimama mahali pale pale. Mungu amjalie mtoto wako apone, utamtumikia maisha yako yote, na uwe Mkristo mashuhuri na umtumikie Yeye. Wewe na mumeo, pia.

311 Je, utaliahidi, huko nyuma, baba, pia? Ikiwa Mungu atamwacha mtoto wako aishi, unaahidi utamtumikia? Mkono wake umeinuliwa kwa Mungu. Utafanya vivyo hivyo.

312 [Dada huyo anaendelea kuongea—Mh.] Sawa. Sasa, sasa nenda, na wewe na mume wako mkamtumikie Bwana. Na Mungu ambariki mtoto na apone. Amina. Mungu akubariki, dada.

Itieni hiyo alama kwenye vitabu vyenu sasa.

Njoo, ndugu, Ndugu Neville.

54-1219M Uponyaji Wa Kiungu
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org